# UKRISTO NI NINI?
## (What Is Christianity?)

**Na**
**Joel  Stephen Williams, MTh, PhD**

*"Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe"* (Marko 16:15).

Mzalishaji/Producer
**Worl Evangelism Team**

Nakala ya Kiswahili/Swahili Copy
**Swahili Gospel Team** (SGT)

**HAKIUZWI**
NOT FOR SALE

# UKRISTO NI NINI?

***"Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohubiriwa"***
(1 Wakorintho 1:21).

***"Bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi"***
(1 Wakorintho 1:23).

***"Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu"***
(2 Wakorintho 4:5).

Mawasiliano/Contacts:
+255 (0) 765 098 981
+255 (0) 764 792 979

## YALIYOMO

Ukristo ni Nini . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .1
Hitaji la Wokovu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 2
Mwokozi kutoka Mbinguni . . . . . . . . . .. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 5
Kuzaliwa kwa Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 7
Maisha ya Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 9
Mafundisho ya Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .12
Kutokuwa na Dhambi kwa Kristo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 14
Upatanisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 16
Kufufuka kwa Kristo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 20
Kuokolewa kwa Neema . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 23
Imani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 25
Toba . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 27
Utii . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 28
Hiari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 29
Ubatizo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 30
Maisha ya Kikristo. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 35
Kanisa . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 39
Huduma na Uinjilisti . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 44
Ibada . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 46
Wakati Ujao . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 53
Utatu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .58
Roho Mtakatifu na Miujiza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .61
Maandiko Matakatifu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 63
Muhtasari wa Vitabu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 65
Agano la Kale . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 65
Agano Jipya . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .67
Hitimisho . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .69

# Vifupisho

## Baadhi ya Maandiko ya Agano la Kale

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mw. | Mwanzo | isa. | Isaya |
| Kum. | Kumbukumbu la Torati | Yer. | Yeremia |
| Zab. | Zaburi | Eze. | Ezekieli |

## Maandiko ya Agano Jipya

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mt. | Mathayo | 1 Tim. | 1 Timotheo |
| Mk. | Marko | 2 Tim. | 2 Timotheo |
| Lk. | Luka | Tit. | Tito |
| Yn. | Yohana | Flm. | Filemoni |
| Mdo. | Matendo ya Mitume | Ebr. | Waebrania |
| Rum. | Warumi | Yak. | Yakobo |
| 1 Kor. | 1 Wakorintho | 1 Pet. | 1 Petro |
| 2 Kor. | 2 Wakorintho | 2 Pet. | 2 Petro |
| Gal. | wagalatia | 1 Yoh. | 1 Yohana |
| Efe. | Waefeso | 2 Yoh. | 2 Yohana |
| Flp. | Wafilipi | 3 Yoh. | 3 Yohana |
| Kol. | Wakolosai | Yud. | Yuda |
| 1 The. | 1 Wathesalonike | Ufu. | Ufunuo |
| 2 The. | 2 Wathesalonike | | |

Msomaji anahimizwa kuwa ama na Agano Jipya au Biblia nzima na kusoma marejeo yote ya Maandiko ambayo yameandikwa katika kitabu hiki. Zaidi ya Biblia, chanzo pekee ambacho kitanukuliwa itakuwa kamusi ya Kiyunani, kwa kuwa Agano Jipya awali liliandikwa kwa Kiyunani: *Kamusi ya Kiyunani kwa Kiingereza ya Agano Jipya na kitabu kingine cha Kikristo*, kilichoandikwa na Walter Bauer. kilichotafsiriwa na kuhaririwa na William F. Arndt, F. Wilbur Gingrich, na Frederick W. Danker. Chicago: Chuo Kikuu cha Chicago Press, 1979.

# Ukristo ni Nini?

Ukristo ni nini? Lengo la kitabu hiki ni kukuelezea kuhusu Ukristo kwa maneno rahisi, ili kukuonyesha unavyoweza kufanyika Mkristo, na kufupisha kile ambacho ni lazima uamini na unavyopaswa kutenda kama Mkristo. Ukristo ambao utausoma katika kurasa zinazofuata ni Ukristo kama ulivyojulikana na kufanywa katika kipindi cha mitume wa karne ya kwanza. Jaribio la dhati litafanywa kuandika kwa usahihi kutoka katika Maandiko Matakatifu kila dai lililotolewa kuhusu Ukristo. Kinachofuata ni jaribio la kuwasilisha kwako Ukristo bila nyongeza yoyote ya mapokeo ya wanadamu kutoka miaka 2,000 iliyopita. Ingawa baadhi ya mapokeo hayo hayakuwa na madhara, baadhi yalikuwa na makosa na yanapaswa kuepukwa.

Watu wengi leo hii wanachanganyikiwa kuhusu Ukristo ni nini hasa kwa sababu wanauhusisha na mapokeo ambayo yanauficha ukweli. Labda umewahi kubaguliwa kwa ajili ya Ukristo kipindi kilichopita, kwa sababu uligeuzwa na mfano usiofaa kanisani, au maisha ya baadhi ya watu wanaojiita Wakristo. Kama jambo hili ni la kweli kwako, tafadhali soma kitabu hiki na uhukumu Ukristo kwa ubora unaopaswa kuwa, si jaribio lisilofaa la baadhi ya watu kuwa Wakristo. Hukumu Ukristo kwa misingi tuliyopewa katika Agano Jipya kwa kile ambacho Wakristo na kanisa linapaswa kufanya. Wale wanaodai kuwa ni Wakristo hawawezi kuishi, kuabudu, au kufundisha kama wanavyopaswa kwa sababu mbalimbali. Labda hawaujui ukweli wote. Labda wamepotoshwa na mafundisho ya uongo. Labda ni wanafiki. Inawezekana ni waaminifu, lakini wamekosea kama wanadamu wote wanavyokosea. Tafadhali usiukatae Ukristo kwa sababu ya kukosea kwa mtu unayemjua anayedai kuwa ni Mkristo. Uhukumu Ukristo kwa kumtazama Yesu Kristo. Utagundua kuwa Yesu Kristo, Mwanzilishi wa dini ya Kikristo, hatakukatisha tamaa kwa namna yoyote ile. Wakati wafuasi wake wanakosea, yeye hana kosa.

## Hitaji la Wokovu

Ukristo ni dini ya wale wanaoitwa "Wakristo" (Mdo 11:26; 1Pet. 4:16). Mkristo ni mfuasi wa Yesu wa Nazareti ambaye anaitwa Kristo au Masihi. Kwa nini kila mmoja anapaswa kuwa Mkristo? Jibu la swali hili ni kwamba tunahitaji wokovu kwa ajili ya dhambi zetu. Ili kuelewa hitaji letu la wokovu kutoka dhambini, kwanza kabisa tujue inamaanisha nini kwa mwanadamu ambaye anawajibika na kuhesabiwa mbele za Mungu.

Binadamu wote ni zaidi ya viumbe vyenye mwili kama vile Wanyama. Tuna kitu kilichopo ndani yetu ambacho kinaitwa "roho" au "nafsi," ambayo inamaanisha viumbe wa kiroho (Mdo 7:59; 1Kor. 2:11; 1The. 5:23; Yak. 2:26). Hii inamaanisha kwamba Mungu ametupa uwezo wa kufikiri na kuamua. Tuna uwezo wa kufahamu mambo ya kiroho na kumwamini mtu mkuu tunayemwita "Mungu." Tunaweza kujua jema na baya, kuwa na hatia, pamoja na kuyaelewa mambo ambayo ni yenye heshima na matakatifu. Tuna uwezo wa kuhisi hisia ya hofu tunapotafakari ukuu wa Mungu. Tuna uwezo wa kuabudu, na kila mahali ulimwenguni, makabila na tabaka za watu wote, himizo la kumfikia mtu mkuu katika ibada ni la watu wote. Tunaweza kuishi maisha matakatifu kwa kuiga ukamilifu mtakatifu wa Mungu (Mt. 5:48; Efe. 4:21-23; 1Pet. 1:14-16).

Mtume Paulo alipokuwa akihubiri huko Athene, Ugiriki, aliwasifu Waathene kwa kuwa watu wa "kidini sana" (Mdo 17:22). Walikuwa na madhabahu na vitu vya kuabudu miungu tofauti tofauti. Ili waweze kuhakikisha kuwa hawakusahau miungu yoyote, walijenga madhabahu ya ***"kwa mungu asiyejulikana"*** (Matendo 17:23). Hivyo, Paulo akawataarifu Waathene hao kuhusu Mungu pekee wa kweli:

> "Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono; wala hatumikiwi kwa mikono ya

wanadamu kana kwamba anahitaji kitu cho chote; kwa maana ndiye anayewapa wote uzima na pumzi na vitu vyote. Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani, na mipaka ya makazi yao; ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone, ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu. Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu. Kama vile mmoja wenu, mtunga mashairi alivyosema, Maana sisi sote tu wazao wake" (Matendo 17:24-28).

Kwa kuwa Mungu ndiye mwumbaji wetu, tunawajibika kwake (Isa. 43:7; Ufu. 4:11). Paulo aliwaambia Waathene kuwa siku moja watahukumiwa na Mungu: ***"Anawaamuru watu wote wa kila mahali watubu, kwa sababu ameiandaa siku ambayo ulimwengu utahukumiwa kwa haki"*** (Mdo 17:30). Kwa kuwa Mungu ametupa uwezo wa kuamua na kujua jema na baya, tunawajibika kwake. Paulo alizungumza kuhusu watu ambao hawakuwa na sheria yoyote iliyoandikwa kutoka kwa Mungu; hata hivyo "kwa asili walijua sheria inahitaji nini" (Rum. 2:14). Kwa kuwa tuna uwezo wa kujua Mungu yupo (Zab. 19:1-6; Rum. 1:19-20), na kwa kuwa tuna uwezo wa kujua jema na baya, lazima tutoe hesabu ya mawazo, matendo na maisha yetu mbele za Mungu (Mdo 10:42; Rum. 2:16; 1 Kor. 4:5).

Ukweli unaohuzunisha ni kwamba binadamu wote waliokuwa wakubwa na wakaweza kujua tofauti kati ya mema na mabaya wamefanya dhambi. Dhambi ni chochote kile kilicho kinyume na mapenzi ya Mungu. Dhambi ni "uasi" (1 Yoh. 3:4). ***"Kila lisilo la haki ni dhambi"*** (1Yoh. 5:17). Mema na mabaya hayaamuliwi kiholela na Mungu. Badala yake, kile kilicho sawa kwa Mungu ni sahihi na kile kisicho sawa kwa Mungu ni kosa. Mungu ni upendo, hivyo, kutokuwa na upendo ni dhambi (1Yoh. 4:8, 16). Ukweli ni sahihi, kwa kuwa Mungu hajawahi kudanganya (Tit. 1:2). Kuna orodha nyingi za aina

tofauti za dhambi katika Agano Jipya ambazo zinatusaidia kuelewa zinahusu nini. Katika Warumi, Paulo ameandika kuhusu wenye dhambi:

> "Wamejawa na udhalimu wa kila namna, uovu na tamaa na ubaya; wamejawa na husuda, na uuaji, na fitina, na hadaa; watu wa nia mbaya, wenye kusengenya, wenye kusingizia, wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutakabari, wenye majivuno, wenye kutunga mabaya, wasiowatii wazazi wao, wasio na ufahamu, wenye kuvunja maagano, wasiopenda jamaa zao, wasio na rehema;" (Warumi 1:29-31).

Paulo pia ameorodhesha baadhi ya "matendo ya mwili" au dhambi: ***"Uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo"*** (Gal. 5:19-21). Paulo anaorodhesha mifano kadhaa ya wale ambao hawatarithi mbinguni, isipokuwa wakitubu na kutafuta wokovu. Hii inahusisha ***"waasherati, waabuduo sanamu, wazinzi, wafiraji, walawiti, wevi, watamanio, walevi, watukanaji, wanyang'anyi"*** (1Kor. 6:9-10; Kol. 3:5-10; 1 Tim. 1:9-11; 2Tim. 3:2-5; Yak. 3:14-16; 1Pet. 2:1-2).

Hatuwezi kuwalaumu wengine kwa sababu ya dhambi zetu. Tunatenda dhambi kwa sababu tunajiingiza katika majaribu (Yak. 1:12-15). Ingawa Adamu na Hawa walileta dhambi ulimwenguni, lakini hatujawahi kulazimishwa kufanya dhambi. Tumefanya dhambi kwa sababu tumefuata mfano wa wengine na kwa kuwa tumetamani kufanya lile lililo ovu. Hivi ndivyo ambavyo dhambi ilivyoenea kwa wanadamu wote (um. 5:12). Kama vile wote waliomfuata Kristo wameokoka, vivyo hivyo, wote waliomuiga na kumfuata Adamu katika njia za dhambi wamepotea (Rum. 5:15-21). Baadhi ya watu wanafundisha uongo kuwa tunarithi dhambi ya asili kutoka kwa Adamu, na kwamba wote tuna hatia ya dhambi mara tu baada ya kuzaliwa. Biblia inafundisha tofauti. Kila mtu yeye binafsi atawajibika

mbele za Mungu. Watoto hawatahukumiwa kuwa wana hatia kwa ajili ya dhambi za wazazi wao au kwa ajili ya dhambi za Adamu. Vile vile, wazazi hawatahukumiwa kwa ajili ya dhambi za watoto wao (Yer. 31:29-30; Eze. 18:1-20). Kila mmoja atawajibika peke yake kwa Mungu.

Kwa kuwa sisi ni wenye dhambi na kwa kuwa Mungu ni Mtakatifu na Mkamilifu, tunatengwa naye (Isa. 59:1-2). Adamu na Hawa walitupwa nje ya Bustani ya Eden baada ya kufanya dhambi (Mw. 3:1-24). Kila mtu ana hatia ya dhambi mbele za Mungu, hata watu wa kidini (Rum. 3:9). ***"Hakuna mwenye haki hata mmoja"*** (Rum. 3:10). ***"Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu"*** Rum. 3:23; 1Yoh. 1:8-10). Malipo ambayo wote tunastahili kwa ajili ya dhambi zetu ni kifo. ***"Mshahara wa dhambi ni mauti"*** (Rum. 6:23; Gal. 6:7-8). Katika hili tunaona hitaji letu la wokovu. Tumepotea, kwa sababu ni wenye dhambi. Hatuwezi kujiokoa wenyewe. Hatuna msaada (Rum. 5:6). Kama tunajaribu kwa bidii, tunaweza kufanya dhambi kidogo, lakini bado tutafanya dhambi. Zaidi ya yote, hatutaweza kulipa deni la dhambi ambazo tumeshazifanya. Tunahitaji sana wokovu. Tunamuhitaji mwokozi!

## Mwokozi Kutoka Mbinguni

Fikiria mtu amekwama chini ya shimo refu. Hawezi kutoka. Anahitaji msaada kutoka nje au kutoka juu. Anahitaji mtu amrushie kamba au ngazi. Anahitaji mwokozi. Mwanadamu yupo katika hali ya namna hiyo kwa sababu ya dhambi zetu. Tunahitaji msaada kutoka mbinguni, na Mungu wetu mkuu ametupatia Mwokozi. Kuna Mungu mmoja tu (Kum. 6:4; Mk. 12:29, 32; 1 Kor. 8:4, 6; Efe. 6:6; Yak. 2:19), lakini huyu Mungu anatambulika kwetu kwa njia tatu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu (Mt. 28:19; 2Kor. 13:14; Yn. 15:26). Kumwita Mungu "Baba" hakumaanishi Mungu alioa au kwamba yeye na mke wake wa mbinguni walikuwa na mtoto. Neno "Baba" linatuambia kuwa

Mungu ni kama baba kwa kuwa anatuangalia na kutujali (Mt. 6:9; 7:9-11). Yesu Kristo hakuitwa “Mwana wa Mungu” kwa sababu Mungu na mke wake wa mbinguni walimzaa, au kwa sababu Baba ni mkubwa kuliko Mwana. Aliitwa “Mwana wa Mungu” kwa sababu alikuwa mtiifu katika uhusiano wake na Mungu Baba kama vile mtoto yeyote anavyokuwa mtiifu kwa baba yake (Yn 4:34; 5:30; 6:38). Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu wote ni wa milele na wote ni Mungu, si wanadamu.

Hii inamaanisha kuwa Mwokozi wetu, Yesu Kristo, maisha yake hayakuanza au kuwepo alipozaliwa hapa duniani. Aliishi kabla ya Ibrahimu (Yn. 8:58). Alikuwepo kabla ya kuumbwa ulimwengu (Yn. 1:3; Kol. 1:15-16; Ebr. 1:2). Hii inajulikana kama uwepo wa Kristo tangu awali (Yn. 3:13; 8:23; 17:5, 24; 18:37). Mwokozi wetu Yesu Kristo ni wa milele. Alikuwepo siku zote na siku zote atakuwepo (Ufu. 1:8, 17; 21:6; 22:13; Yn. 1:1; Ebr. 13:8). Ingawa alikuwa mbinguni mahali ambapo malaika wengi wangeweza kumwokoa, kwa hiari alikuja ulimwenguni ili awe Mwokozi wetu (2Kor. 8:9). Paulo anaelezea Habari njema za ajabu ambazo zinafanya hadithi ya Ukristo kuwa ya kipekee sana. ***“Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu;”*** (Wafilipi 2:5-7).

Mwanadamu mwenye dhambi alihitaji mwokozi. Badala ya kuomba kisichowezekana kwetu, ambacho ni, kulipa dhambi zetu wenyewe, Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee duniani kutatua tatizo la dhambi kwa ajili yetu (Yn. 3:16). Ndio maana ujumbe wa Kristo unaitwa “injili” (Mk. 1:1; 16:15; Rum. 1:16; Efe. 1:13; 1 Tim. 1:11). Neno “injili” linamaanisha “habari njema.” Ni habari njema kwa kuwa hali yetu haikuwa na tumaini. Mungu amemtuma kwetu Mwokozi ili

atuokoe kutoka dhambini. Wokovu umetujia kutoka mbinguni kupitia Mwana wa Mungu, Yesu Kristo.

## Kuzaliwa Kwa Kristo

Ili Mwana wa Mungu awe Mwokozi wetu, Mungu aliandaa uzao maalum na wa kimuujiza utokee. Mungu alimchagua mwanaume na mwanamke mzuri wa Kiyahudi, Yusufu na Mariamu, wawe wazazi wa mtoto huyu maalum. Yusufu na Mariamu walichumbiana, ina maana waliahidiana na walichukuliwa kama mume na mke, lakini walikuwa hawajaanza kuishi pamoja na walikuwa hawajakamilisha ndoa yao kwa kukutana kimwili (Mt. 1:18-25). Mariamu alikuwa bado ni mwanamwali (Lk 1:26-34). Kwa miujiza Mungu alimuumba mtoto Yesu tumboni mwa Mariamu kupitia Roho Mtakatifu (Mt. 1:20; Lk 1:35). Kwa namna hiyo Yesu alikuwa na mama wa kimwili, lakini Mungu alikuwa Baba yake (Gal. 4:4; Rum. 1:3; Lk. 1:35). Huku ndiko huwa kunaitwa "kuzaliwa kwa Yesu na mwanamwali."

Neno linalotumika mara kwa mara kuelezea hatua hizi zote ni "kufanyika kuwa mwili." Neno hili linamaanisha Mwana wa Mungu alifanyika kuwa mwanadamu. Mtume Yohana alitumia msamiati "Neno" akimaanisha Yesu anapoelezea kuzaliwa kwa mwili: ***"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu…Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu"*** (Yn 1:1, 14, Rum. 8:3; 1 Tim. 3:16; 1Yoh. 4:2; 2Yoh. 7). Ili aweze kuwa mwokozi wetu kamili, Kristo alikuwa mmoja wetu (Ebr. 2:14, 17).

Yesu Kristo ni wa pekee kwa namna nyingi, na asili zake mbili, ubinadamu na uungu, kuunganishwa na kuwa kiumbe kimoja ni muhimu sana. Alipokuwa angali hapa duniani, Yesu Kristo alikuwa mwanadamu kabisa. Alishuka kutoka mbinguni na alizaliwa na mwanadamu (Mt. 1:1-7; Rum. 1:3; 9:5). Alipitia hatua za ukuaji wa

kawaida ambazo wanadamu wote wanazipitia. Alikuwa mtoto mchanga ambaye aliongezeka na kuwa kijana (Lk 2:40). Alikuwa na mahitaji ya kimwili ya kawaida ya mwanadamu ya chakula, maji, na kupumzika. Pia alikuwa na hitaji la kusali (Mt. 4:2; 8:24; 14:23; Yn. 4:5-7; 19:28). Kama mwanadamu, Yesu alikuwa na hisia kama vile furaha, huzuni, hasira, upendo, na huruma (Mt. 9:36; 26:37; Mk. 3:5; 10:21; Lk 10:21; Yn. 12:27; 15:11). Yesu alilia pia (Yn 11:35) na alijaribiwa (Mt. 4:1-11; Lk 4:1-13; Ebra. 4:15). Yesu alihisi maumivu ya mwili na kupitia kifo kama mwanadamu. (1Pet. 3:18; 4:1). Ndio, Yesu alikuwa mwanadamu kabisa.

Wakati huo huo, hata hivyo, Yesu alikuwa Mungu kabisa (Yn. 10:30). Hakuitwa tu "Bwana" na "Mwana wa Mungu," ambayo yalitumika kama majina ya Uungu (Yn 10:25-33; Lk 2:11; Ufu. 4:8-11; 19:16), pia aliitwa "Mungu" (Yn 1:1; 20:28; na labda Rum. 9:5; Tit. 2:13; Ebr. 1:8; 2Pet. 1:1;). Ingawa Yesu hakutumia kabisa nguvu zote zinazohusiana na yeye kuwa "Mungu" alikuwa sehemu Uungu (Kol. 1:15; 19:2-9). Yesu Kristo alikuwa Mungu katika mwili. Alikuwa Mungu na mwanadamu kwa wakati mmoja. Rangi nyeusi na nyeupe zikichanganywa pamoja, matokeo yanakuwa katikati, rangi ya kijivu. Lakini Yesu hakuwa wa katikati kati ya Mungu na mwanadamu. Hakuwa malaika. Alikuwa Mungu na mwanadamu kwa wakati huo huo.

Kwa kuwa Yesu alikuwa ni Mungu na mwanadamu, ni Mwokozi kamili. Anaweza kutuwakilisha au kutupatanisha kikamilifu katika sehemu zote katika agano kati ya Mungu na mwanadamu (1Tim. 2:5-6). Kama mwanadamu aliweza kulipa deni la dhambi zetu. Kama Mungu alikuwa mkamilifu na dhabihu inayostahili kulipia deni la dhambi zetu. Tutajifunza jambo hili zaidi katika sura zinazofuata tunapoendelea kuzungumzia upatanisho, lakini ni muhimu kujua kwamba yote yalikuwa ni mpango wa Mungu tangu kuumbwa kwa ulimwengu (1Pet. 1:20). Kwa kuwa Yesu alipaswa kuwa Mungu na Mwanadamu kwa wakati mmoja, alikuja duniani kwa njia ya uzao wa

pekee kupitia mama wa kimwili na Baba wa mbinguni. Mwokozi wetu alikuja kutoka Mbinguni, na Mwokozi huyo ni Mwana wa Mungu. Kama wachungaji walivyoambiwa: ***“Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo, Bwana”*** (Lk. 2:11).

## Maisha ya Kristo

Kama hujui sana kuhusu maisha ya Kristo, itakulazimu usome vitabu vinne vya Injili, Mathayo, Marko, Luka, na Yohana. Vitabu hivi vinne vinatuambia kuhusu kuzaliwa kwa Yesu (Mat. 1:1-2:12; Lk 1:26-2:20) na mojawapo ya tukio alipokuwa na umri wa miaka kumi na mbili (Lk. 2:41-52). Lakini msisitizo wa vitabu hivyo upo katika miaka mitatu au minne ya maisha ya Yesu ambayo ilikuwa ni huduma yake ya wazi. Tangu kipindi alipokuwa na umri wa miaka thelathini, Yesu alihubiri na kufundisha watu mapenzi ya Mungu. Aliwavutia wanafunzi wengi, na akachagua wafuasi maalum, walioitwa “mitume,” ambao walihubiri ujumbe wake baada ya kuondoka kwake hapa duniani.

Yesu alifanya miujiza mingi ambayo ni uthibitisho kuwa Mungu amethibitisha kile alichokisema na kile alichokuwa anakifanya (Yn. 2:11; 5:36; 10:25, 37-38; 14:11; Lk. 7:20-22; Mt. 9:1-8; Ebr. 2:4). Miujiza michache tu ya Yesu imesimuliwa katika vitabu hivi vinne vya Injili, lakini ***“hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake”*** (Yn. 20:30-31). Ifuatayo ni orodha ya miujiza ya Yesu katika Injili nne:

1. Kubadilisha maji kuwa divai (Yohana 2:1-11).
2. Kumponya mtoto wa diwani (Yohana 4:46-54).
3. Kumponya mtu katika Sinagogi (Marko 1:23-26; Luka 4:33-35).
4. Kumponya mama mkwe wa Petro (Mt. 8:14-15; Mk. 1:30-31; Lk. 4:38-39).
5. Kuvua samaki wengi kwa mara ya kwanza (Luka 5:1-11).

6. Kumponya mkoma (Mt. 8:2-4; Mk 1:40-42; Lk 5:12-13).
7. Kumponya mtu aliyepooza (Mt. 9:2-7; Mk 2:3-12; Lk 5:18-25).
8. Kumponya mgonjwa katika birika la Bethzatha (Yn. 5:1-9).
9. Kumponya mtu mwenye mkono uliopooza (Mathayo 12:10-13; Marko 3:1-5; Luka 6:6-10).
10. Kumponya mtumishi aliyepooza (Mt. 8:5-13; Lk 7:1-10).
11. Kumfufua mtoto wa mjane (Luka 7:11-15).
12. Kuponya vipofu wawili (Mathayo 9:27-31).
13. Kuyatuliza mawimbi (Mt. 8:23-27; Mk 4:37-41; Lk 8:22-25).
14. Kuponya watu wawili wenye pepo (Mathayo 8:28-34; Marko 5:1-15; Luka 8:27-35).
15. Kumponya mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu (Mathayo 9:20-22; Marko 5:25-29; Luka 8:43-48).
16. Kumfufua binti wa Yairo (Mathayo 9:18-19, 23-25; Marko 5:22-24, 38-42; Luka 8:41-42, 46-56).
17. Kumponya mtu bubu, mwenye pepo (Mathayo 9:32-33).
18. Kuwalisha watu 5,000 (Mathayo 14:15-21; Marko 6:35-44; Luka 9:12-17; Yohana 6:5-13).
19. Kutembea juu ya maji (Mt. 14:25; Mk 6:48-51; Yn. 6:19-21).
20. Kumponya binti wa mwanamke Mkananayo (Mathayo 15:21-38; Marko 7:24-30).
21. Kumponya kiziwi mwenye utasi (Marko 7:31-37).
22. Kulisha kwa miujiza watu 4,000 (Mt. 15:32-38; Mk 8:1-9).
23. Kumponya kipofu (Marko 8:22-26).
24. Kumponya kijana mwenye pepo (Mathayo 17:14-18; Marko 9:17-19; Luka 9:38-43).
25. Kutoa shekeli mdomoni mwa samaki (Mathayo 17:24-27).
26. Kumponya mtu aliyezaliwa kipofu (Yohana 9:1-41).

27. Kumponya mtu aliyekuwa kiziwi na kipofu (Mt 12:22; Lk 11:!4).
28. Kumponya mwanamke kilema (Luka 13:11-13).
29. Kumponya mtu mwenye safura (Luka 14:1-4).
30. Kumfufua Lazaro (Yohana 11:1-44).
31. Kuwaponya watu kumi wenye ukoma (Luka 17:11-19).
32. Kuwaponya vipofu wawili (Mt 20:19-34; Mk 10:46-52; Lk 18:35-43).
33. Kuunyausha mtini (Mt. 21:18-22; Mk 11:12-14, 20-25).
34. Kurudishia sikio la mtumishi wa Kuhani Mkuu lililokatwa (Luka 22:50-51).
35. Kuvua samaki wengi kwa mara ya pili (Yohana 21:1-11).

Injili hizi nne pia zinatuelezea kuhusu ubatizo wa Yesu (Mt. 3:13-17; Mk 1:9-11; Lka 3:21-22). Yesu hakubatizwa kwa sababu ya dhambi yoyote ambayo ilihitaji msamaha. Alibatizwa kwa sababu ilikuwa ni jambo la haki kulifanya ili kumtii Mungu. Alijitambulisha kwetu ili awe Mwokozi wetu. Katika ubatizo wake sauti ya Mungu kutoka mbinguni ilisikika ikisema ***"Huyu ni Mwanangu, mpendwa, ninayependezwa naye"*** (Mt. 3:17). Vitabu hivi vya Injili pia vinatuambia kuhusu kujaribiwa kwa Yesu mara tu baada ya ubatizo (Mt. 4:1-11; Lk 4:1-13). Tukio moja la muhimu katika maisha ya Yesu linaitwa "Kubadilika sura" (Mt. 17:1-8; Mk. 9:2-10; Lk. 9:28-36; 2 Pet. 1:16-18). Katika tukio hili Yesu alibadilika mbele ya mitume wake watatu Petro, Yakobo na Yohana. Aling'aa sana kwa mwonekano wake, labda kwa sababu Uungu wake ulijitokeza. Sauti kutoka mbinguni ikasikika ikisema: ***"Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, msikieni yeye!"*** (Mk. 9:7). Karibia na mwisho wa maisha ya Yesu tunasoma kuingia kwake kwa ushindi Yerusalem (Mt. 21:1-11; Lk 19:28-40; Yn. 12:12-19), kusafisha kwake hekalu (Mt. 21:12-17; Mk. 11:15-19; Lk. 19:45-48), na kukamatwa kwake, kujaribiwa, kusulibiwa, na kufufuka

kwake (Mt. 26:36-28:10; Mk. 14:32-16:18; Lk. 22:39-24:49; Yn 18:1-21:14).

## Mafundisho ya Kristo

Wakristo wanamtaja Yesu kama Mwalimu Mkuu. Kwa jinsi tunavyojua, Yesu hakuwa na elimu rasmi (Yn. 7:15); hata hivyo, alifundisha kwa namna ambayo watu walimshangaa (Yn. 7:46). Wakati mwingine Yesu alifundisha kwa mifano au hadithi ambazo zilifanya mafundisho yake yawe ya kuvutia. Alitumia mifano ya kawaida ya kila siku katika maisha ya watu na kuitumia katika mafundisho yake. Tofauti na walimu wengi ambao walishindwa katika baadhi ya vipengele kuyaishi yale wanayoyafundisha (Mt. 23:3), Yesu aliyaishi kikamilifu yale aliyokuwa akiyafundisha. Yesu alifundisha akiwa na mamlaka kuu (Yn. 3:34; 7:16; Mt. 7:28-29). Hakuhitaji kukata rufaa kwenye mamlaka yoyote ya watu ili kihakikishwe kile alichokisema. Angeweza kuthibitisha kirahisi tu kwa kusema: ***"Nawaambieni"*** (Mt. 5:22, 28, 32, 34, 39, 44). Yesu alifundisha ukweli tu, yeye alikuwa kweli. Aina ya maisha ambayo Yesu anatufundisha tuishi ni aina ya maisha ambayo yatatuongoza katika furaha (Yn. 10:10; Mt. 5:3-12). Wanasaikolojia wengi wamegundua kuwa kile walichowaambia watu wakifanye ili wawe na furaha ni sawa na kile ambacho Yesu aliwafundisha watu muda mrefu uliopita.

Baadhi ya mifano ya Yesu ilikuwa ni ya ajabu kwa sababu ya uzuri wake. Soma, kwa mfano, mifano mitatu katika kitabu cha Luka 15. Mfano wa Kondoo aliyepotea, Sarafu iliyopotea na Mwana mpotevu. Mifano hii inatuambia kuwa Mungu anatuhitaji sisi watoto wake tuliopotea, turudi nyumbani na atatukaribishe. Pia soma habari za mchungaji mwema katika kitabu cha Yohana 10. Baadhi ya mafundisho makuu ya Bwana wetu Yesu yamekusanywa pamoja katika vipindi virefu katika Injili ya Mathayo. Soma vipengele vitatu vinavyofuata vya

mafundisho ya Yesu na utaona ni kwa nini ameitwa kwa usahihi kuwa ni Mwaliku Mkuu.

1. Hotuba ya mlimani (Mathayo 5:1-7:28).
2. Mfano wa ufalme (Mathayo 13:1-53).
3. Maisha katika ufalme (Mathayo 18:1-35).

Fundisho la kimaadili la Kristo ni jambo lililo kuu sana ambalo ulimwengu haujalitambua. Kiwango cha maadili ambacho Yesu alifundisha hakikuwa kanuni za nje za sheria na kanuni. Alienda kwenye kiini cha tatizo (Mt. 23:1-28). Kuua ni kosa, lakini Yesu alitufundisha tutoe chuki na hasira mioyoni mwetu pia, kwa sababu itatupeleka kwenye tendo lenyewe la kuua (Mt. 5:21-26). Tendo la uzinzi ni kosa, lakini Yesu alitufundisha kuepuka tamaa mioyoni mwetu (Mt. 5:27-30). Yesu alitufundisha kutenda matendo mema, lakini tunapaswa kuyafanya kwa nia njema (Mt. 6:1-6, 16-18). Tendo jema linalofanywa kwa ubinafsi linapoteza uzuri wake wote. Mafundisho mengi ya Yesu yalihusu ***"ufalme wa Mungu"*** (Mk. 1:14-15; Mt. 13:1-53). Mara nyingi ***"ufalme wa Mungu"*** unahusu kutawala au utawala wa Mungu. Yesu anapozungumza kuhusu kurithi ufalme, anamaanisha kupokea kwetu thawabu ya Mbinguni na uzima wa milele (Mt. 25:34). Kwa kuzungumza kuhusu ufalme wa Mungu mara kwa mara, Yesu alikuwa akiwahamasisha watu kujikabidhi kwa Mungu kama Mfalme na kumtii katika mambo yote (Mt. 6:10). Yesu alisisitiza pia toba, unyenyekevu na kuwatumikia wengine (Mk 1:15; 9:35; 10:15; Lk. 22:25-27).

Yesu alisisitiza kwa umakini mkubwa sana kuhusu upendo kama msingi wa kuishi maisha sahihi. Kwa "upendo" Yesu hakumaanisha "kujisikia vizuri kuhusu mtu fulani" au "kumpenda mtu fulani." Upendo ambao aliuzungumzia ulikuwa ni kutafuta kile ambacho ni bora zaidi kwa mtu mwingine kwa namna ambayo si ya kibinafsi. Alisema

kwamba tuwapende pia maadui zetu (Mt. 5:43-48). Mtu yeyote anaweza kuwa mwema kwa mtu ambaye ni mwema pia kwake, lakini je, tunaweza kuwa wema kwa mtu ambaye ni adui yetu? Yesu aliwafundisha wanafunzi wake "kupendana" (Yn. 13:34; linganisha na Yn. 15:10; 1Yoh. 5:3; 2Yoh. 6). Alifundisha kuwa upendo ni wajibu mkuu kwa mwanadamu: ***"'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote.' Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, 'Mpende jirani yako kama nafsi yako'"*** (Mt. 22:37-39; linganisha na Mk. 12:29-30; Lk. 10:27; Kum. 6:5). Yesu alitupa kile ambacho kilikuja kuitwa "sheria ya dhahabu" ya maisha: ***"Basi yoyote mtakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo"*** (Mt. 7:12; Lk. 6:31). Bila shaka Yesu anayo ***"maneno ya uzima"*** (Yn. 6:68).

## Kutokuwa na Dhambi kwa Yesu Kristo

Maandiko yanazungumzia kuhusu Yesu "kufanywa mkamilifu" (Ebr. 5:9). ***"Dhambi haimo ndani yake"*** (1Yoh. 3:5). Kama dhabihu ya mwana-kondoo Yesu hakutakiwa kuwa na mawaa (Y. 1:29; Ebr 9:14). Mtume Petro alisema: ***"Yeye hakutenda dhambi"*** (1Pet. 2:22). Mtume Paulo aliandika: ***"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu"*** (2Kor. 5:21). Yesu ***"alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi"*** (Ebr. 4:15). Yesu alithubutu hata kuwauliza wapinzani wake; ***"Ni nani miongoni mwenu anishuhudiaye ya kuwa nina dhambi?"*** (Yn. 8:46). Hakika Yesu Kristo ni "Mtakatifu na mwenye Haki" (Mdo 3:24). Yesu hakuwa na dhambi, hivyo, hakuwahi kukosea na alikuwa mwema na mwenye haki (Mdo 10:38).

Ushahidi wa Yesu kutokuwa na dhambi ulikuwa wa mbali kabisa. Ulikuja tu kutoka kwa marafiki wenye huruma ambao walielekea kutia chumvi, lakini pia ulikuja kutoka kwa watu ambao hawakuwa upande wowote wa Yesu. Cha kushangaza zaidi, ushahidi pia ulikuja kutoka

kwa wale ambao hawakumhurumia. Hapa kuna ufupisho wa ushahidi wa Yesu kutokuwa na dhambi:

1. Mashahidi waliokuwa na huruma
   A. Petro – Lk 5:8; 1Pet. 1:19; 2:22; 3:18; Yn. 6:69; Mdo 3:14.
   B. Yohana – 1 Yohana 2:1, 29; 3:5, 7; Matendo 4:27.
   C. Paulo – 2 Wakorintho 5:21.
   D. Mwandishi kwa Waebrania – Waebrania 2:10; 4:15; 5:8-9; 7:26, 28; 9:14.
   E. Stefano – Matendo 7:52.
   F. Anania – Matendo 22:14.
   G. Wakristo wa kwanza – Matendo 4:30.
   H. Malaika Gabriel – Luka 1:35.
2. Mashahidi wasio na huruma.
   A. Viongozi wa Kiyahudi – Mathayo 26:55-59; Marko 14:48-56; Luka 22:52-53; Yohana 18:20-21.
   B. Yuda – Mathayo 27:4.
   C. Pepo – Marko 1:24; Luka 4:34.
3. Mashahidi wasiokuwa na upande wowote.
   A. Pilato – Mathayo 27:18, 23-24; Marko 15:14; Luka 23:4, 14-15, 22; Yohana 18:38; 19:4-6.
   B. Mke wa Pilato – Mathayo 27:19.
   C. Mwizi msalabani – Luka 23:41.
   D. Askari – Luka 23:37.
4. Ushahidi wa Yesu mwenyewe.
   A. Yohana 8:46; 14:30; 15:25; 18:23.
   B. Utii wake mkamilifu – Yohana 4:34; 5:30; 6:38; 7:18; 8:29, 55; 15:10; 17:4; Luka 22:42; Waebrania 10:5-7.

Ushahidi wa Yesu mwenyewe unaweza kuwa wa thamani kuliko yote. Kadiri watu wanavyokuwa bora, ndivyo wanavyoelekea kufahamu makosa madogo madogo katika maisha yao wenyewe. Kadiri watu wanavyokuwa waovu, ndivyo wanavyoekusudia kupunguza dhambi kubwa katika maisha yao. Utu wa ndani wa Yesu hautudhibitishii kuwa alitambua dhambi au kosa lolote katika maisha yake. Kwa yeye kudai kwamba hakuwa na dhambi iwe ilikuwa ni mojawapo ya madai ya majivuno ambayo hayajawahi kufanywa na mtu yeyote, au ilikuwa ni kweli. Yesu alikuwa ama kichaa, mwongo au Bwana. Ushahidi mwingine ulipelekea kuthibitisha dai la Yesu kutokuwa na dhambi, hivyo, Wakristo wanaamini kuwa alikuwa mkamilifu na bila mawaa. Sasa tutaona umuhimu mkubwa wa Yesu kutokuwa na dhambi tunapoziangalia kazi zake kama dhabihu ya upatanisho wa dhambi zetu.

## Upatanisho

Neno “upatanisho” lina reelea ufunikaji wa dhambi uliokamilishwa kwa kifo cha Yesu pale msalabani. Kama hujasoma kuhusu mateso na kifo cha Yesu msalabani, tafadhali fanya hivyo kutoka katika mojawapo ya vitabu vya Injili (Mt. 27:27-52; Mk. 15:16-39; Lk. 23:26-48; Yn. 19:16-37). Katika kipindi cha Musa Mungu alikuwa akiwatayarisha wanadamu kuuelewa kuhusu upatanisho kupitia dhabihu tofauti tofauti ambazo aliwaamuru Wayahudi kutoa (Rum. 15:4; 1Kor. 10:6). Kwa mfano, kifo kilipokuwa kikiwachukuwa wazaliwa wa kwanza wa kila familia huko Misri, wana wa Israeli waliamriwa kutoa dhabihu ya mwana-kondoo asiye na kasolo. Walitakiwa kupaka damu ya mwana-kondoo huyo kuzunguka milango yao. Nyumba ambazo zilikuwa na damu juu ya mlango zilikuwa salama, watoto hawakuuawa. Mungu alikuwa anatuonyesha kwa njia ya mifano kile

ambacho atakifanya kijulikane zaidi baadaye. Tunaweza kuepuka kifo cha milele kwa njia ya damu ya Yesu.

Somo lingine kutoka katika Agano la Kale kuhusu upatanisho linapatikana katika sikukuu ya Kiyahudi ya Upatanisho. Wayahudi walitumia mbuzi wawili. Mmoja alikuwa anatolewa dhabihu na damu ilinyunyizwa hekaluni. Halafu kuhani mkuu ataweka mikono yake juu ya mbuzi yule mwingine, wakati mwingine walimwita mbuzi wa Azazeli. Kuhani atazikiri dhambi za watu, ikimaanisha kuzihamishia dhambi zao kwenda kwa mbuzi asiye na hatia. Halafu mbuzi huyo atapelekwa jangwani. Hivyo, watu wataelewa kuwa dhambi zao zimeondolewa. Kumwaga damu pamoja na kuutoa uhai ilikuwa njia ya kuoshwa dhambi. ***"Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo"***(Ebr. 9:22). Kristo ni dhabihu yetu ya upatanisho na ni Mwana-kondoo wetu wa Azazeli ambaye alichukua dhambi zetu na kuziondoa: ***"Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa"*** (1Pet. 2:24).

Dhabihu za Agano la Kale, ambazo nyingi zilikuwa ni za wanyama, hazikuwa suluhisho kamili kwa tatizo la dhambi za mwanadamu. Zilikuwa ni za muda tu wakati Mungu alikuwa anaandaa kumtuma Mwanawe ulimwenguni (Gal. 3:23-25; 4:4). Zilikuwa zimeundwa ili kumfundisha mwanadamu utii na kuamini katika ahadi za Mungu. Zilikuwepo ili kutufundisha dhana ya dhabihu, kwa uhai mmoja kutolewa ili kuupatanisha mwingine. Tunaambiwa na mwandishi kwa Waebrania kwamba ***"maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi"*** (Ebr. 10:4). Lakini damu ya Yesu na dhabihu ya uhai wake usio na hatia pale msalabani iliweza kuondoa dhambi zetu. Wakati Yohana Mbatizaji alipomwona Yesu, alisema: ***"Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!"*** (Yn. 1:29). Kuliko kutoa dhabihu ya mnyama kwa ajili ya

dhambi ya ulimwengu, Yesu alijitoa yeye mwenyewe: ***"lakini sasa, mara moja tu, katika utimilifu wa nyakati amefunuliwa azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake"*** (Ebr. 9:26).

Somo lingine kubwa kuhusu upatanisho kutoka katika Agano la kale linapatikana katika kitabu cha Isaya 52:13-53:12, likijulikana kama mojawapo ya vifungu vya mateso ya mtumishi. Kifungu hiki kinamhusu Yesu katika Agano Jipya (Mdo 8:32-35). Katika Isaya 53 yule aliyekuwa Mtumishi wa Mungu alikuwa hana hatia kama vile Yesu alivyokuwa hana dhambi (Isa 53:7, 9). Mateso ya Mtumishi huyu yalikuwa kamili, kama yalivyokuwa mateso ya Yesu (Isa. 53:5, 8, 12). Mateso ya Mtumishi huyu hayakuwa ya bahati mbaya, bali yalikuwa yamepangwa na Mungu, kama yalivyokuwa mateso ya Yesu (Isa 53:6, 10; Mdo 2:23; 1Pet. 1:20). Mateso ya Mtumishi huyu yalikuwa mabaya, kama yalivyokuwa mateso ya Yesu (Isa. 53:4-6, 12; 2Kor. 5:21). Hatimaye mateso ya Mtumishi huyu yakawa mabaya, tena, kama yalivyokuwa mateso ya Yesu (Isa. 53:11-12; Rum. 8:37; 1Kor. 15:54-57). Katika kifo cha Kristo tunapata ushindi wa dhambi, kifo na Ibilisi (Ebr. 2:14; Kol. 2:14-15). Yesu alitabiri kifo chake katika maneno: ***"Hii ni damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi"*** (Mt. 26:28). Paulo alisema kifo cha Yesu kilikuwa dhabihu ya upatanisho katika damu yake (Rum. 3:25). Petro anawaambia Wakristo kuwa wamefidiwa, yaani, wamenunuliwa kutoka katika utumwa wa dhambi, ***"kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo"*** (1 Pet. 1:19). Ni kwa damu ya Yesu ambayo alijitoa fidia akamnunulia ***"Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa"*** (Ufu. 5:9; linganisha na Efe. 1:7; 5:25; Mk 10:45; Mdo 20:28; 1Kor. 6: 19-20; 1Yoh. 1:7).

Kifo cha Yesu kilikuwa ni kwa ajili ya watu wote. Baadhi ya watu wanafundisha kimakosa kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya wale waliochaguliwa na Mungu tu ili waokolewe. Wanasema upatanisho

unampaka, lakini Biblia inasema kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya ulimwengu wote (Yn. 1:29; 3:16-17; 4:42; 2Kor. 5:19; 1Yoh. 2:2; 4:14). Aliwafia "watu wote" (2Kor. 5:14; 1Tim. 2:6; Ebr. 2:9; Tit. 2:11), pia kwa ajili ya wenye dhambi (1Tim. 1:15; Rum. 5:6-8) na wale ambao walishaokolewa lakini sasa wamepotea (2Pet. 2:1). Hii inaendana na tabia ya Mungu ambaye anataka watu wote waokolewe (2Pet. 3:9; 1Tim. 2:4). Ingawa Yesu alikufa kwa ajili ya watu wote, si watu wote wataokolewa. Upatanisho upo kwa ajili ya kila mtu, lakini ni baadhi tu wataamini na kuokolewa (1 Tim. 4:10).

Njia kuu ambazo kwa hizo kifo cha Yesu kinapatanisha dhambi zetu ni mabadilishano. Yesu hakuwa na dhambi. Alikuwa mkamilifu, bila dosari wala doa. Hakustahili kuteseka na kufa. Ingawa hakustahili kifo, alichukua nafasi yetu na kuzibeba dhambi zetu yeye mwenyewe. Alikufa kwa ajili yetu katika nafasi yetu. Alimturudisha katika ushirika na Mungu, akaondoa utengano kati yetu na Mungu ambao ulisababishwa na dhambi (Isa. 59:1-2). Kama Petro alivyoelezea: ***"kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, ili atulete kwa Mungu"*** (1Pet. 3:18). Paulo anaelezea upatanisho kwa undani:

> "Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye. Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake" (Warumi 5:6-10).

Hii ndiyo sababu Kristo ndiye tumaini la pekee la wokovu kwa ajili ya wenye dhambi: ***“Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo”*** (Mdo 4:12). Hakuna atakayemfikia Baba ila kupitia Kristo (Yohana 14:6).

Mshahara wa dhambi ni mauti (Rum. 6:23), lakini Mungu hakuhitaji kifo cha mtu asiye na hatia tofauti na mapenzi ya mtu binafsi. Mungu hakumwambia mwanadamu: “Mtoe dhabihu mtoto wako mchanga kwa ajili ya dhambi zako.” Badala yake, Mungu Mwana alifanyika kuwa mwanandamu kwa njia ya mwili na kuzaliwa na mwanamwali. Mungu mwenyewe, kwa namna ya Mwana, aliishi maisha makamilifu, bila kufanya dhambi. Mungu mwenyewe alitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu. Upendo wa Mungu ulionekana kwa njia ya kifo cha Yesu msalabani (Yn 3:16; Rum. 5:8; Efe. 5:25). Hii ndiyo sababu inayowafanya Wakristo waweke msisitizo katika kuhubiri kuhusu kifo cha Yesu pale msalabani (1Kor. 1:23; 2:2; 15:1-4; Gal. 6:14). Kama Wakristo tunashukuru kwa zawadi kuu ya Mungu ya kumtoa Mwanawe. Tunaguswa na upendo wa Mungu, ili tuhamasishwe na kutiwa moyo tuishi maisha matakatifu (Mk 8:34-37; 1Yoh. 4:19; 2Kor. 5:14-15; Yn. 12:32; 15:13; Flp. 3:10; 1Pet. 2:21; Flp. 2:5-8; Ebr. 12:1-3). Kama Wakristo hatujivuni au kufikiri kuwa sisi ni watu maalum. Tunajivuna na kujisifu katika Kristo kwa sababu ya kile alichokifanya kwa ajili yetu (Gal. 6:14; 2Kor. 4:5).

## Kufufuka kwa Kristo

Baada ya Yesu kufa msalabani, alizikwa kaburini na jiwe kubwa lililofunga mlango wa kaburi. Askari wakawekwa kama walinzi nje ya kaburi. Asubuhi ya siku ya kwanza ya juma, hata hivyo, Yesu alifufuka na kuliacha kaburi (Mt. 28:1-15; Mk. 16:1-18; Lk 24:1-49; Yn 20:1-29; Gal. 1:1; Efe. 1:20). Usichanganye ufufuo wa Yesu na fundisho la

kuzaliwa upya au uhamisho wa roho. Hatuzaliwi na kuzaliwa tena na tena katika miili tofauti tofauti tunapoishi maisha tofauti tofauti. Tunaishi na kufa mara moja (Ebr. 9:27). Baadaye tutafufuliwa kutoka wafu ili tusimame mbele za Mungu katika hukumu na kuona mwisho wetu wa umilele utakuwaje (Yn. 5:29).

Kuna sababu mbalimbali kwa nini Wakristo wanaamini kuwa Yesu alifufuka. Kaburi lake lilikuwa tupu, na mwili haukuibiwa (Mdo 2:29; Mt. 28:13). Zaidi ya yote, kulikuwa na mashahidi wengi waliomwona Yesu akiwa hai baada ya kufufuka (Mdo 2:32; Yn 20:27-28; 1kor. 15:4-7). Badiliko la ajabu lililotokea katika maisha ya watu wengi, limeelezewa vizuri kwa kufufuka kwa Kristo. Ni kwa sababu ya kufufuka kwa Kristo kwamba wengi waliamini wakati wengine wakiongeza ujasiri wa kuhubiri (Yn 5:7; Mdo 1 :14; 4:13-21; 5:42). Uongofu wa Sauli wa Tarso, ambaye baadaye alijulikana kama mtume Paulo, unaelezewa vizuri na kufufuka kwa Yesu Kristo (1Kor. 15:8-10; Mdo 9:1-22; 22:1-16).

Tunapaswa kupokea kwa imani ukweli wa kufufuka kwa Yesu (Yn. 20:27; Rum.10:9-10). Tunapaswa kubatizwa kwa kufuata kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Bwana wetu (Rum. 6:1-6; Kol. 2:12; 1Pet. 3:21). Tunapaswa kusukumwa kutaka kumwabudu Kristo kama matokeo ya kufufuka kwake, kwani inathibitisha kuwa yeye ni Bwana (Mt. 28:9, 17; Rum. 1:4; Yn. 20:28). Ni lazima tuhisi furaha kuu, kwa kuwa ufufuo wake unatupa tumaini (Mt. 28:8; Yn. 20:20; Rum. 6:9). Ufufuo wake ni uthibitisho kutoka kwa Mungu kwamba tutafufuliwa kutoka wafu ifikapo mwisho wa dunia (Rum. 8:29; 14:9; 1Kor. 15:20, 23, 51-54; Efe. 2:6; Kol. 1:18; 2Tim. 1:10; Ufu. 1:5, 17-18). Bila kufufuka kwake, tumepotea na kila tunachokifanya katika jina lake ni bure (1Kor. 15:14-19). Ni kwa kupitia kufa na kufufuka kwa Yesu, Mungu ametoa wokovu kwa ajili yetu (Rum. 4:25; 1Pet. 3:21). Ikiwa “tunamjua Yesu na nguvu ya wokovu wake,” tutapata kufufuka kutoka wafu” na

makao huko mbinguni (Flp. 3:10; linganisha na Yn. 14:19; Rum. 8:11; 1Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14; 1The.4:14; 1 Pet. 1:3).

Kanisa la kwanza lilihubiri sana kuhusu msalaba wa Kristo, pia walihubiri sana kuhusu kufufuka kwa Kristo (Mdo 2:24, 31; 4:2, 10; 5:30; 13:30-33, 37; 26:22-23). Kwa kweli, hii ni sehemu muhimu ya kazi ya kanisa, inayoitwa, kuhubiri kufufuka kwa Yesu kutoka wafu (Lk 24:48; Mdo 1:8, 2:32; 3:15; 4:33; 5:32; 10:39-41; 13:47; 1Kor. 11:26).

Kufufuka kulifuatwa na kupaa kwa Yesu Kristo kwenda mbinguni (Lk 24:50-53; Mdo 1:6-11). Kupaa kulimaanisha mwisho wa baada ya kufufuka kwa Yesu, na lilikuwa tukio la kuinuliwa mbinguni na Mungu Baba (Mdo 2:32-36; 7:56; Kol. 3:1-2; Ebr. 1:2; 8:1). Baada ya kuzungumza kuhusu kifo cha Yesu msalabani, Paulo alisema kuhusu kupaa kwa Kristo: ***"Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba"*** (Wafilipi 2:9-11).

Kwa sababu ya maisha yake makamilifu na dhabihu ya kifo chake, Mungu alimfufua kutoka kaburini na kumpa mamlaka yote mbinguni na duniani (Mt. 28:18). Kristo amefanywa kuwa kichwa cha kanisa (Efe. 1:20-23; Kol. 1:16-18; Mdo 4:11; 1Pet. 2:7; Mk 12:10). ***"Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi"*** (Mdo 5:31). Hii inamaanisha kuwa Yesu yupo hai, yupo katika nafasi ya mamlaka kuu, na ana uwezo wa kuomba kwa niaba yetu mbinguni (Rum. 8:34; Ebr. 1:3; 7:25; 8:11, 34; 1Yoh. 2:1). Yesu hajafanyika kuwa kitu chochote bali Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana (Lk 1:32-33; Ufu. 17:14; 19:16). Tunapoiangalia nafasi ya Yesu mbinguni akiwa mkono wa kuume wa Mungu, tunapaswa kumtii Mungu na kuziweka akili zetu katika mambo ya kiroho badala ya mambo ya duniani (Wakolosai 3:1-2).

## Kuokolewa kwa Neema

Kwa sababu tulistahili kifo na hukumu kwa ajili ya dhambi zetu, wokovu lazima uwe kwa neema ya Mungu. Neema kwa kawaida inamaanisha "upendeleo usiostahili." Labda hadithi nzuri sana kuwahi kusimuliwa ambayo inaelezea neema ni kisa cha Mwana Mpotevu (Lk 15:11-32). Huyu mtoto alichukua urithi wake na kuondoka nyumbani. Akatumia fedha zake katika maisha ya dhambi. Alipoishiwa fedha na kuteseka kwa njaa, aliamua kurudi nyumbani na ikiwezekana apate kazi kama mtumwa kwa baba yake, lakini baba yake alimkaribisha nyumbani na akamfanya tena kuwa mwanawe.

Haiwezekani sisi kupata au kustahili wokovu wetu. Hatuwezi kuzilipia dhambi zetu; hatuwezi kumweka Mungu kwenye nafasi ambayo atakuwa na deni kwetu. Tunaweza kumfanyia Mungu kazi, na kutenda matendo mema, lakini tayari tunawajibu wa kuwa wema, hivyo, hakuna sifa maalum katika hili. Hata kama tumekuwa wema, tuko kama watumwa katika mojawapo ya mifano ya Yesu: ***"tumefanya tu yaliyotupasa kufanya"*** (Lk 17:10). Hiki ndicho kile ambacho Biblia inamaanisha pale inaposema hatuwezi kuokolewa kwa matendo (Gal. 2:16). Kama wokovu ulikuwa ni kwa matendo, tungedaiwa, na usingekuwa tena zawadi kwa neema ya Mungu (Rum. 4:1-8). Kama Paulo alivyosema: ***"Lakini ikiwa ni kwa neema, haiwi kwa matendo tena, au hapo neema isingekuwa neema"*** (Rum. 11:5-6; linganisha na 2Tim. 1:9).

Ili tuweze kuokolewa lazima tuwe wanyenyekevu. Kama tungeweza kujiokoa wenyewe kwa nguvu zetu wenyewe kwa namna fulani, tusingeweza kuwa wanyenyekevu, bali tungejivuna. Tungejisifu na kujivuna kwa kile tulichokifanya ili kuokoka. Hii ndio maana tunaweza kuokolewa kwa neema tu, ili kujivuna kuondolewe (Rum. 3:27; Efe. 2:8-9). Mtume Paulo ni mfano mzuri wa mtu mwenye sababu za kujivunia uwezo na mafanikio ya mwanadamu (2Kor. 11:1-

12:13). Lakini Paulo alisema: ***“Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo”*** (1Kor. 15:10). Paulo alijisifia nini? Alijisifia kuhusu upendo wa Mungu ulioonyeshwa katika Kristo Yesu: ***“Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu cho chote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo”*** (Gal. 6:14). ***“Yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana”*** (1Kor. 1:31; linganisha na 2Kor. 10:17).

Wokovu unapatikana kwa Mungu kama zawadi ya bure, kwa kuwa ni kwa neema. Paulo alisema ***“tunahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu”*** (Rum. 3:24). ***“Bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu”*** (Rum. 6:23; linganisha na 2Kor. 9:14-15; Ufu. 22:17). Kama wokovu ni bure na ni zawadi, je, hiyo inamaanisha tusifanye chochote ili tuokolewe? Hili si kweli, na sehemu yote iliyobaki ya kitabu hiki nitashirikiana nawe katika kile ambacho unapaswa kufanya. Lakini kwa muda mchache hebu tuone kwa nini tunapaswa kufanya kitu kwa ajili ya wokovu ingawa ni zawadi ya bure ya neema ya Mungu.

Ingawa wokovu ni zawadi, ni muhimu kwetu kuupokea na kuufanya uwe na ufanisi katika maisha yetu. Tumeokolewa kwa neema, lakini neema huja “kupitia imani” (Efe. 2:8). Kama tutakavyoona katika kurasa chache zijazo, ni lazima pia tutubu na kumtii Mungu kama tunataka kuokolewa. Ni kitu gani hasa kinachotuokoa? Kielelezo rahisi kinaweza kuelezea hili linaloonekana kuwa na utata. Hebu fikiria kuwa ni mchana na upo pamoja na marafiki wawili katika chumba kilicho na dirisha. Unawauliza marafiki zako kwa nini kuna mwanga chumbani. Rafiki yako mmoja anasema: “Kwa sababu kuna dirisha.” Rafiki mwingine anasema: “Kuna mwanga chumbani, kwa kuwa jua linaangaza nje.” Ni rafiki yupi yupo sahihi? Wote wako sahihi. Jua ni chanzo halisi cha mwanga, lakini dirisha inawezekana ni njia ambayo mwanga wa jua unaweza kuingia chumbani. Jua linasababisha mwanga, lakini mwanga unakuja kupitia dirishani.

Wokovu wetu upo hivyo hivyo. Kama vile jua linavyosababisha mwanga, kitu hasa kinachotuokoa sisi ni Mungu, Kristo, Roho Mtakatifu, damu ya Yesu, na neema ya Mungu. Lakini Mungu hawezi kuulazimishia wokovu kwa mtu. Ni lazima tutoe viambata sahihi "ambavyo" kupitia hivyo neema ya Mungu huja katika maisha yetu ili ituokoe. Ni dirisha gani ambalo ndani yake wokovu wa Mungu hufikia roho zetu? Ni "imani" (Efe. 2:8; Rum. 5:1-2). Ni kama tutakavyoona kuhusu toba. Ni utii. Pia ni ubatizo ambao tutajifunza kwa undani muda mfupi ujao. Hatupati wala kustahili chochote tunapobatizwa. Ni njia tu ambayo kwayo au kupitia hiyo Mungu anatuokoa. Kama Paulo alivyoandika: ***"alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa na kuzaliwa kwa pili*** *(ubatizo)* ***na kufanywa upya na Roho Mtakatifu"*** (Tit. 3:5; linganisha na Mdo 2:38; 22:16; 1 Pet. 3:21).

Kuokolewa kwa neema si jambo ambalo linamaanisha kusitisha juhudi katika upande wetu kuwa wema na kuishi maisha matakatifu. Tusiichukulie neema ya Mungu kirahisi. Lazima tusidhani kuwa tutafanya dhambi tunavyotaka, na Mungu atatusamehe moja kwa moja (Rum. 6:1-2; 2 Pet. 2:17-22; Yuda 4). Tunahitimisha sehemu hii ya neema kwa kauli ya Paulo ya fundisho; ***"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zetu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu"*** (Efe. 2:8-9).

## Imani

Kwa kuwa tumeokolewa "kwa imani" (Efe. 2:8; Rum. 1:6), ni muhimu kuielewa dhana hii muhimu. Yesu alisema: ***"mtakufa katika dhambi zenu; kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye"*** (Yn. 8:24; linganisha na Mdo 15:9). Lazima tuamini kuwa Mungu yupo (Ebr. 11:6). Lazima tuamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu (1Yoh. 5:1;

Rum. 10:9-10). Tumeahidiwa kuwa kama tutamwamini Yesu, hatutahukumiwa, bali tutakuwa na uzima wa milele (Yn 3:16, 18, 36; 6:35; 11:26; 20:30-31; Mdo 10:43; 16:31). Tunahesabiwa haki kwa imani (WRum. 3:24, 28; 5:1; Gal. 2:16; 3:24). Kwa kuwa imani ni muhimu kwa ajili ya wokovu, imani ni nini?

Imani, huanza na maarifa. Inaanza kwa mtu kutoa kibali cha kiakili kwa ukweli fulani. Paulo aliuliza: ***"Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema! Lakini si wote walioitii ile habari njema. Kwa maana Isaya asema, Bwana, ni nani aliyeziamini habari zetu? Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo"*** (Rum. 10:14-17).

Basi imani huanza kwa kusikia kuhusu Mungu na Yesu Kristo na kukubali ukweli fulani unaowahusu. Lakini aina ya imani inayookoa ni zaidi ya hili. Huu ni mwanzo tu. Kwa mfano, ninaweza kuamini kuwa mwanamke fulani ni daktari, ambaye amepitia mafunzo, na kwamba uchunguzi wa ugonjwa wangu ni sahihi. Ninaweza kuamini kuwa dawa atakazonipa zitaponya ugonjwa wangu. Imani yote hiyo itakuwa ni ya bure, kama sitamwamini daktari na kuchukua dawa. Vivyo hivyo, imani ni kuamini kuwa Mungu yupo, lakini imani ile isiyomwamini na kumtii Mungu si imani kamili. Kama Yakobo alivyosema: ***"Mashetani nao wanaamini na kutetemeka"*** (Yak. 2:19). Mashetani wanaamini kuwa Mungu yupo. Pia wanaogopa hata nguvu za Mungu na wanatetemeka kwa hofu, lakini hawamtii Mungu na hawajaokolewa.

Aina ya imani inayookoa ni imani inayohusisha matendo. Imani inayookoa ni kujitolea na kutenda kile unachoamini kuwa ni kweli. Ona jinsi hili linavyooneshwa na mashujaa wa imani (Ebr. 11:1-38). Ikiwa imani yetu imewekewa kikomo cha kukubali kiakili, itakuwa ni imani iliyokufa na haitatuokoa (Yak. 2:14-26). Imani yetu lazima iwe hai na inayofanya kazi (Gal. 5:6). Baadhi ya watu watakuambia kuwa kile

unachotakiwa kufanya ili uwe Mkristo ni maelezo mafupi kwamba umwamini Yesu kama Mwana wa Mungu. Lakini kumwamini Yesu au kuwa na imani katika yeye ina maana sana zaidi ya hiyo. Hii ina maana kwamba unabadilisha utii wako, vipaumbele vyako na mwelekeo wa maisha yako. Ni lazima uishi kwa imani kwa kumfuata Yesu kila siku na kumtii. ***"Amwaminie Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia"*** (Yn 3:36).

## Toba

Toba ni sehemu kuu ya mahubiri ya Yesu kuhusu ufalme wa Mungu (Mt. 3:2; 4:17; Mk. 1:15; 6:12). Ilikuwa ni sehemu iliyohubiriwa mara kwa mara na kanisa la kwanza (Mdo 2:38; 3:19; 26:20). Kabla ya Yesu kupaa mbinguni, alisema kuwa ***"toba na msamaha wa dhambi lazima ihubiriwe kwa mataifa yote katika jina lake"*** (Lk 24:47). Kwa sababu dhambi ni ya ulimwengu wote, toba pia inapaswa kuwa ya ulimwengu wote. Paulo alisema kuwa Mungu ***"anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu"*** (Mdo 17:30). Toba ni ya muhimu kwa sababu ni sehemu ya muhimu ya vile tunavyopaswa kufanya ili tuokolewe (Mdo 2:38; 3:19; 11:18). Ndio maana Mungu anataka watu wote watubu, na kwa uvumilivu anatupa nafasi mbalimbali za kututubu (2Pet. 3:9). Mtu mwenye dhambi akitubu, huleta furaha mbinguni (Luka 15:7;10).

Toba ni nini? Neno la Kiyunani la neno "toba" linamaanisha "badiliko la akili, majuto, kugeuka, uongofu, mwanzo wa dini na maisha yenye maadili." Toba inahusisha huzuni kwa ajili ya dhambi zetu. Paulo alisema: ***"Huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba iletalo wokovu lisilo na majuto"*** (2Kor. 7:10), lakini watu wengi wamechanganyikiwa katika sehemu hii. Kuna aina mbalimbali za huzuni. Watu wengi wana huzuni wamekamwatwa na dhambi. Baadhi

ya watu wana huzuni kwa kuwa wameadhibiwa kwa sababu ya dhambi zao. Ikiwa huzuni yetu haiendi mbali zaidi ya hii, basi hatujatubu. Toba inamaanisha kuwa tuna huzuni ya kutosha kiasi cha kubadilisha tabia. Ina maana kwamba tuna huzuni vya kutosha kujitolea kufanya vizuri zaidi (Mt. 21:28-31). Tunabadili mwelekeo wa maisha yetu. Angalia ni mara ngapi katika Biblia watu wanatiwa moyo kutenda kwa namna ambayo itajulikana na wengine kuwa wametubu (Mdo 3:8; Lk 3:8; Mdo 26:20). Toba ni rahisi kuielezea, lakini sio rahisi kuifanya. Ni hatua ambapo tunaacha kuishi kwa ajili ya nafsi zetu.

## Utii

Kama mtoto atamwambia baba yake kuwa anampenda, lakini hamtii, matendo yake hayaendani na upendo anaosema anao (Mdo 21:28-31). Utii kwa Kristo na Mungu si hiari. Katika uchambuzi wa mwisho, utii ni wa muhumu ikiwa tutampenda Mungu au Kristo. Hakuna njia nyingine ya kuonyesha kuwa unampenda Mungu zaidi ya kumtii: ***"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake"*** (1Yoh. 5:3; linganisha na 1Yoh. 2:5; 2Yoh. 6). Yesu alisema: ***"Mkinipenda, mtazishika amri zangu"*** (Yn. 14:15: linganisha na Yn. 15:10). Tunasafisha roho zetu kwa kuitii kweli (1Pet. 1:22). Wokovu ni kwa wale wanaotii Ebr. 5:9; Mdo 10:34-35). Hukumu ya Mungu itakuwa juu ya wale wasioitii Injili ya Yesu Kristo (2 The. 1:7-9).

Kwa kusema tu kirahisi kuwa unampenda na kudai kuwa unamfuata Bwana haitoshi. Yesu alisema: ***"Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni"*** (Mt 7:21). Kama unafikiri kumtii Mungu ni kazi ngumu, usikate tamaa. Utii hakika ni muhimu kwa ajili ya wokovu wetu, lakini si tatizo linaloshindikana kwa mtu anayeamini kweli ambaye anampenda Bwana. Yohana anatuambia kwamba "amri za Mungu si nzito" (1Yoh. 5:3).

Utakapotambua kile Kristo alichofanya kwa ajili yako kwa kuja hapa duniani na kufa msalabani, utataka kumtii, na utafanya hivyo kwa furaha.

## Hiari

Wokovu ni zawadi ya bure kwa neema ya Mungu, lakini una masharti. Injili inahubiriwa, lakini watu lazima waamini, msamaha unatolewa bure, lakini ni lazima tutubu. Mungu ni wa rehema, lakini ni lazima tuwe watiifu. Wokovu umeshalipwa kwa dhabihu ya upatanisho ya Yesu Kristo, lakini itakuwa na ufanisi katika maisha ya wale waliojitoa katika mapenzi ya Mungu. Katika Biblia yote watu wamepewa chaguzi mbili ziitwazo njia ya uzima, na njia ya mauti (Kum. 30:15; Mdo 2:40). Tumepewa uhuru wa kuchagua njia tunayotaka kupita. Tunaweza kumfuata Yesu au kumkataa (Yn 14:6; Mt 11:28-30). Mungu ametupa vishawishi vingi vya kufanya yaliyo sawa. Kinyume chake anayafanya maisha ya dhambi kuwa matupu ili kutuchochea tutubu, lakini Mungu hatulazimishi kufanya jema au baya.

Ukweli kwamba tumeamriwa kuamini, kutubu, na kutii, hiyo inamaaisha kwamba tuna hiari. Baadhi ya watu wanafundisha kimakosa kwamba mwanadamu hana hiari na kwamba watu wote walishapangiwa tangu awali kuwa wamtii Mungu au kuishi katika uasi wa dhambi. Watu wengine wanakosea kufundisha kuwa Mungu ameshampangia kila mtu tangu awali kwamba aokolewe au apotee na kwamba hatuna uhuru wa kuchagua hatima yetu. Lakini kama Mungu atatuwajibisha kwa ajili ya dhambi zetu, ni lazima iwe kwa sababu tumechagua kwa hiari kutokumtii yeye. Biblia inafundisha kuwa tunaweza kuchagua kati ya jema na baya (Yak. 4:17; Yn 7:17; Mdo 13:46). Mungu anatuita katika maisha ya utii yatakayotuletea wokovu (1The. 2:12; 1Tim. 6:12; Ebr. 9:15; 1Pet. 2:9), na wito huu umetolewa kwa njia ya kuihubiri injili (2The. 2:14). Tunachagua kuitikia wito wake

kwa toba, ambayo ni badiliko la akili, nia na moyo. Mungu hajaamua kama tutaamini au tusitubu. Biblia imeweka wazi kuwa Mungu amefanya baadhi ya chaguzi hata kabla hajaumba ulimwengu. Mungu alichagua kuwa Kristo atakuja duniani kutuokoa kutoka dhambini (Mdo 2:23; 1Pet. 1:18-20). Biblia pia inasema kuhusu kuchaguliwa tangu asili, lakini haihusishi kuchagua mmoja kuokolewa na mwingine apotee. Sio uchaguzi wa mtu mmoja mmoja bali ni uchaguzi wa jumla wa tabaka fulani au aina ya watu binafsi. Mungu alichagua kuwa wale wanaomwamini Kristo na wale watakaoishi aina fulani ya maisha wataokolewa (Rum. 8:28-30; Efe. 1:4-5, 11; 2The. 2:13; 1Pet. 1:2-3).

Linganisha fundisho la kuchaguliwa na mwalimu wa shule. Kama mwalimu atachagua ni wanafunzi gani wafaulu na wanafunzi gani wafeli bila kuwapa nafasi ya kusoma na kufanya majaribio, hii itakuwa sio haki. Hata hivyo, kama mwalimu ataamua kuwa wanafunzi wote watakaopata kuanzia 90 hadi 100 watapata daraja la “A”, wale watakaopata kati ya 80 na 89 watapata daraja “B” na kadhalika, hii itakuwa haki. Mungu alichagua tangu awali kuwa wote wanaoamini katika Kristo na wale watakaoishi maisha matakatifu wataokolewa. Wale wanaomkataa Kristo na kuishi maisha ya uasi wa dhambi watapotea. Mungu ametuachia uchaguzi wa aina ya maisha tunayotaka kuishi kwa hiari yetu wenyewe.

## Ubatizo

Ubatizo ni wa muhimu kwa sababu ni hatua ambayo mtu anaingizwa kanisani. Neno “Ubatizo” limetokana na neno la Kiyunani *baptisma* na kitenzi ‘’batiza’’ kutoka katika neno *baptidzo*. Ubatizo unapaswa kufanywa kwa kumzamisha au kumtumbukiza mtu kabisa ndani ya maji. Neno “ubatizo” kwa Kiyunani lina maana ya ‘’chovya, zamisha, batiza’’. Maneno haya ya Kiyunani hayamaanishi ‘’kunyunyiza’’ au ‘’kumwagia.’’ Hata bila ya kujua maana ya maneno ya

Kiyunani, unaweza kujua kwamba ubatizo unapaswa kufanywa kwa kumzamisha au kumchovya mtu kwenye maji. Ubatizo uliashiria kwamba mtu anaufia utu wake wa kale kwa kutubu dhambi. Unapozikwa katika maji ya ubatizo, ule utu wa kale unaachwa ndani ya maji. Unapotoka katika maji ya ubatizo, unafufuliwa katika maisha mapya. Sasa unapaswa kumfuata Kristo kama Mkristo na kuishi maisha ya utauwa na utakatifu (Warumi 6:3-6; Wakolosai 2:12).

Tunajua kuwa katika karne ya kwanza ubatizo ulifanywa kwa kuzamishwa majini, kwa kuwa watu walienda kwenye maeneo tofauti tofauti yaliyokuwa na maji mengi (Yohana 3:23; Marko 1:4-5; Matendo 8:36). Kama ubatizo ungefanywa kwa kunyunyiza, basi yule anayebatiza angeweza kubeba chombo cha maji. Ingekuwa si muhimu kumchukua mtu anayetaka kubatizwa kumpeleka mahali penye maji mengi. Baadhi ya watu wanauliza: ''Maji madogo yana tofauti gani? Suala hapa si kiasi cha maji. Suala ni kwamba, ni lazima tumtii Mungu ambaye alituamuru tuzamishwe. Zaidi ya hayo kuzamishwa kunalingana na ishara ya kuufia utu wetu wa kale wa dhambi, tunapozikwa, na kufufuliwa ili kuishi maisha mapya.

Ni nani anastahili kubatizwa? Ubatizo ni kwa ajili ya wale walioamini na kutubu (Marko 16:16; Mdo 2:38). Ubatizo ni kwa ajili ya wale waliochagua kufanyika kuwa Wakristo na kumfuata Yesu. Watoto hawana umri wa kutosha kuelewa mambo haya. Kumbatiza mtoto, kama makanisa mengi yanavyokosea, inaweza kuwa sherehe ya hisia ambayo ilitokana na mapokeo ya wanadamu, lakini hayaja amriwa na Yesu wala mitume. Mtoto mdogo hahitaji kubatizwa. Mtoto mdogo hana dhambi, hivyo, hana hatia mbele za Mungu (Mt. 18:2-4; 19:13-15; Rum. 9:11; 1 Kor. 14:20; Kumb. 1:39). Watoto wadogo watakaokufa watakwenda mbinguni.

Baadhi ya watu wanadhani Waefeso 2:3 na Zaburi 51:5 zinathibitisha kwamba watoto wamezaliwa wakiwa na dhambi, na hivyo, ni lazima wabatizwe ili kuondolewa hatia ya dhambi ya asili

waliyorithi kutoka kwa Adamu. Lakini wakati Paulo aliandika kuwa Wakristo wa Efeso wakati fulani walikuwa watoto wa hasira'' (Efe. 2:3), hakuwa akizungumzia wakati walipokuwa watoto wadogo.

''Watoto wa'' au ''wana wa'' inamaanisha kuwa mtu fulani anazo sifa kadhaa (Mk. 3:17; Yn. 12:36; Mdo. 4:36; 1The. 5:5; Efe. 2:2; 5:6, 8). Paulo alikuwa akiwazungumzia Wakristo wa Efeso ambao walishakuwa watu wazima. Walizifuata dhambi, hivyo, walikuwa chini ya hasira ya Mungu. Kirai "kwa asili" akimaanishi "kwa kuzaliwa'' (Gal. 2:15; Rum. 11:21, 24), lakini ni hali iliyopatikana ambayo imekuwa kawaida au asili ya pili (1Kor. 11:14; Rum. 2:14). Waefeso waliasili aina ya maisha ya dhambi. Kuishi maisha ya uovu lilikuwa ni jambo la kawaida kwao, lakini hili ni jambo walilolichagua kwa mapenzi yao wenyewe. Haikuwa hali ya upotovu waliozaliwa nayo. Zaidi ya yote, Zaburi 51:5 pekee inafundisha kuwa Daudi alihisi kuwa na dhambi tangu utotoni alipokuja katika ulimwengu wenye dhambi (Isa. 8:8; 1 Sam. 20:30).

Mojawapo ya sababu za msingi za watu wazima kubatizwa ni kuwaruhusu kupokea msamaha wa dhambi zao. Mtoto mdogo hahitaji hili. Tendo lenyewe la ubatizo halina uwezo wa kuokoa. Ni roho ya uaminifu na utii kwenye moyo wa yule anayebatizwa ndio unaojalisha (1Pet. 3:21). Kubatiza mtoto mdogo, ambaye hajui kinachotokea ni bure. Itasababisha kuchanganyikiwa tu baadaye wakati atakapokuwa mtu mzima. Hivyo, ubatizo ni kwa wale wenye umri wa kuweza kuamini, kukiri Imani yao kwa Kristo, kutubu dhambi zao, na kuweza kufanya uamuzi wa kumfuata Kristo (Mt. 28:18-20), kupokea msamaha wa dhambi zao (Mdo. 2:38), kwa ajili ya dhambi zao kuoshwa (Mdo. 22:16; Ebr. 10:22) kupokea makao ya Roho Mtakatifu (Mdo. 2:28; 5:32; Rum. 8:15; 2Kor. 1:22; Gal. 4:6; Efe. 1:13-14), kuokolewa (Mk. 16:15-16; 1Pet. 3:21), kuunganika pamoja na Kristo (Rum. 6:3-6), kumvaa Kristo (Gal. 3:26-27), kuwa mshirika wa kanisa au mwili wa Kristo (Efe. 1:22-23; Mdo. 2:41, 47), kuwa mtakatifu (Efe. 5:25-27), na kuzaliwa upya na kufanywa mpya na Roho Mtakatifu (Yn. 3:5; Tit 3:5).

Tendo la ubatizo lenyewe, mbali na imani na toba, halituokoi. Matendo ya ndani peke yake hayasafishi nafsi au roho ya mtu (1Pet. 3:21; Yn. 3:3-8). Sababu inayofanya ubatizo uwe mzuri ni kwamba tunaiweka Imani yetu katika matendo, tunaamini katika Mungu, tunaliitia jina lake (Mdo. 22:16; Rum 10:13), tunamwomba Mungu kwa dhamiri safi (1Pet. 3:21). Kwa upande wa Mungu ubatizo una maana kwa sababu ametupatia faida ya dhabihu ya damu ya Yesu katika hatua hii (Rum. 6:3-6). Tunapokea tumaini la ufufuo wa uzima kulingana na ufufuo wa Yesu katika hatua ya ubatizo (1Pet. 3:21). Katika historia yote ubatizo umetambuliwa na Wakristo waaminifu kama mpaka unaotenganisha Wakristo na wasio Wakristo, washirika wa kanisa kutoka kwa wasio washirika wa Kanisa, na walio okolewa kutoka kwa wasio okolewa.

Kabla hujabatizwa, unaweza kuwa na kipimo cha Imani katika Kristo na kuwa mfuasi wake kwa kiwango fulani, lakini bado hujaunganika naye (Rum. 6:3-6; Gal. 3:27). Ubatizo ni kama kufunga ndoa. Ndipo mahali unapokiri imani yako katika Kristo na kuahidi kuwa mwaminifu kwake (1Tim. 6:12-13; 1Yoh. 4:2-3, 15; Mt. 10:32-33; Lk. 12:8-9; Rum. 10:9-10). Kabla hujabatizwa unakuwa bado upo nje ya Kristo, na hakuna tumaini nje ya Kristo au mbali na yeye (Efe. 2:12). Katika Kristo, hata hivyo, unazo ***"baraka zote za rohoni"*** (Efe. 1:3), wokovu (2 Tim. 2:10), na msamaha wa dhambi (Efe. 1:7; Kol. 1:14). Ubatizo ni hatua ambapo Mungu anakuondoa kutoka nje ya Kristo na kukuingiza ndani ya Kristo. Ni hatua ambapo unaingia ndani ya Kristo (Rum. 6:3; Gal. 3:27).

Ubatizo ni kwa wale tu wanaomwamini Kristo (Mk .16:16), ambao wamezitubia dhambi zao (Mdo. 2:38), na wale wanaoahidi kuishi kama Wakristo (1Pet. 3:21). Kama unamwamini Yesu Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu, unapaswa kumvaa katika ubatizo ili ufanyike kuwa Mkristo na mshirika wa kanisa lake. Unawezaje kufanya hivyo? Unapaswa kulitafuta kanisa au mhubiri ambaye anafanya

ubatizo wa kuzamisha na kumwomba ubatizwe. Kama utaambiwa ukubaliane na baadhi ya mafundisho ambayo ni tofauti na Biblia, ondoka na utafute kanisa lingine. Kama mhubiri atajaribu kukwambia kuwa ubatizo ni mfano tu wa sherehe na kuwa hauhusiki na wokovu wako, usimwamini. Jifunze tena Biblia yako na kuiamini (Mdo. 2:38; 22:16; Mk. 16:16; 1 Pet. 3:21). Kama hutampata mtu yeyote ambaye atakubatiza kulingana na kweli, unaweza kumwomba rafiki au ndugu yako akubatize.

Biblia haituambii hasa utaratibu kufanya ubatizo au maneno ya kutamka, lakini mbinu ifuatayo itakuwa sahihi, yenye heshima na inayompendeza Mungu. Unaweza kuanza kwa kusali, kukiri kwa Mungu kuwa wewe ni mwenye dhambi, kumwamini Yesu, na kuahidi kufuata ukweli katika maisha yako yote. Wewe pamoja na mtu atakayekubatiza mnaweza kuingia kwenye maji ya mto, bwawa la kuogelea au ziwa. Kama hakuna maeneo yenye maji mengi kama haya, utajaza maji kwenye chombo kikubwa na kutumia. Mtu anayekubatiza anaweza kusema baadhi ya maneno yanayofanana na haya, "Kwa sababu umekiri kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, ninakubatiza kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu" (Mt. 28:19; Mdo. 2:38). Yule anayebatiza anaweza kukuzamisha kwa mbele, kwa nyuma, au kukusukuma chini moja kwa moja, mpaka mwili wako wote uzame kwenye maji kwa muda mfupi. Unapotoka majini, utakuwa ni wakati sahihi wa kumwomba Mungu tena. Unaweza kumshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu kama Mwokozi wako, kumshukuru kwa kuziondoa dhambi zako, na kumwomba akusaidie kukua na kuimarika kama Mkristo.

Mara tu baada ya kubatizwa, unakuwa mtoto mchanga wa Mungu (1Pet. 2:2). Roho Mtakatifu ameingia rohoni mwako kukutakasa, yaani, kukufanya mtakatifu (1Kor. 6:11; Efe. 5:25-27; 1Kor. 3:16-17; 6:19-20). Sasa wewe ni mshirika wa kanisa ambalo Yesu alilifia (Mt. 16:18; Mdo. 20:28). Jina lako limeandikwa katika kitabu cha

uzima, yaani, kitabu cha kukuwekea nafasi kwa ajili ya makao mbinguni (Ufu. 20:15). Dhambi zako zimeoshwa (Mdo. 22:16). Hii haimaaniashi kuwa hautakosea tena (Rum. 7:15-25). Majaribu bado yatakujia. Lakini, kwa kuwa sasa wewe ni Mkristo, hauhitaji kubatizwa tena kila utakapofanya dhambi. Unapofanya dhambi, unapaswa kutubu na kumwomba Mungu ili akusemehe dhambi hiyo (1Yoh. 1:6-10). Pia, unapaswa kutafuta kanisa la Biblia ili uweze kuabudu pamoja na Wakristo wengine ili wakupe moyo. Kwa kuwa umekuwa Mkristo, unapaswa kufanya kama Mkristo, ambalo ni somo la vipengele vichache vinavyofuata.

## Maisha ya Kikristo

Mara tu unapofanyika kuwa Mkristo, unapaswa kuendelea kuishi maisha yanayompendeza Mungu. Kama utageuka mbali na Kristo na ukaanza kuishi tena maisha ya dhambi, utapoteza wokovu wako. Baadhi ya watu hufundisha kimakosa kwamba unapookolewa mara moja, utakuwa umeokolewa katika siku zote haijalishi kile utakachokifanya baadae. Fundisho hili ni kinyume na kile kilichoandikwa katika Biblia (1Kor. 9:27; 10:5-12; Gal. 5:1-4; 1Tim. 4:1, 16; 2Tim. 4:10; Ebr. 3:12; 6:4-8; Yak. 5:19-20; 2Pet. 2:20-22; Ufu. 2:4-5; Lk. 8:11-15; Yn. 15:1-14). Kama hatutapoteza wokovu wetu mara tu tunapookolewa, kutakuwa na ushawishi wa kuishi maisha ya kumcha Mungu. Neema ya Mungu haikutokea kutuokoa sisi tu, bali kuyabadilisha maisha yetu kwa ajili ya mambo mema. Kama Paulo alivyoandika: ***"Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa;"*** (Tito 2:11-12).

Kwa hiyo, unapokuwa Mkristo, unapaswa kuishi vipi? Mara kwa mara katika karne ya kwanza Wakristo wenyewe walisemekana kuwa

na njia (Mdo 9:2; 19:9, 23: 22:4; 24:14, 22). Neno “njia” linamaanisha barabara, “barabara kuu,” lakini katika sitiari inamaanisha “njia ya uzima, namna ya kutenda, mwenendo.” Yesu alisema kwamba yeye ni “njia” (Yn 14:6), ni njia ambayo itatufikisha Mbinguni. Kumfuata Yesu katika maisha yetu ndio namna tunavyoifuata “njia.” Mara kwa mara katika mafundisho ya awali ya Ukristo, njia mbili zimeelezewa. Kuna njia ambayo tunaweza kuishi na njia ambayo hatuwezi kuishi. Kuna njia sahihi na njia potofu, njia ya wema na njia ya uovu, njia ya uzimani na njia ya upotevuni, njia ya Roho na njia ya mwili. Maisha ya Mkristo ni “njia ya haki” (2Pet 2:21: linganisha na Mt. 7:13-14; Lk. 13:23-24).

Kama maisha ya Mkristo ni “njia” kama “njia kuu” au “barabara” basi kuishi maisha ya Kikristo ni kama “kutembea katika barabara hiyo, na mara kwa mara Biblia imetumia neno “enenda” kuelezea maisha ya Ukristo. Mtume Yohana amefupisha jambo hili vizuri: ***“Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda”*** (1Yoh. 2:6). Katika upande hasi tusienende katika mwili, katika dhambi, au katika giza (Rum. 8:4; Efe. 2:1-2; 4:17; Kol. 3:5-7; 2The. 3:6, 11; 1Yoh. 1:6; 2:11). Katika upande chanya tunapaswa kuenenda katika Roho, nuruni, au katika kweli (Rum. 8:4; 2Kor. 5:7; Gal. 5:16; Efe. 2:10; 4:; 5:2, 8, 15; Kol. 1:10; 2:6; 4:5; 1The.2:12; 1Yoh. 1:7; 2Yoh. 4,6; 3Yoh. 3, 4).

Neno lile lile la Kiyunani ni neno la njia “moja ya uzima, mwenendo, tabia.” Wakristo wanapaswa kugeka mbali na maisha yao ya zamani ya dhambi (Efe. 4:22) na kuishi maisha ya kumcha Mungu katika Kristo Yesu (1Tim. 4:12; Yak. 3:13; 1Pet. 1:15; 2:12; 3:1-2, 16; 2Pet. 3:11). Paulo aliliambia kanisa la Efeso ***“mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya”*** (Efe. 4:22; linganisha na Kol. 3:5-9). Badala yake ***“mkavaeutu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli”*** (Efe. 4:24; linganisha na Kol. 3:10). Ni wazi

kwamba kuna aina ya maisha ambayo kama Mkristo unapaswa kuyaishi.

Tunaweza kuelezeaje namna ya maisha ya Mkristo? Si aina ya sheria kama vile amri kumi za Agano la Kale. Sheria zipo kwa ajili ya kutuongoza katika mamlaka kuu ambayo inatupa uhalali wa sheria. Wakati kuna maelezo mengi juu ya kile ambacho unapaswa kufanya na usichopaswa kufanya kama Mkristo, kipimo halisi ni Mungu mwenyewe. Sababu tabia fulani kuwa ni nzuri ni kwamba ni sawa na vile njia ya Mungu inavyosema. Sababu tabia nyingine ni mbaya ni kwamba Mungu Hawezi kufanya hivyo. Paulo alisema "utu wetu mpya" kama Mkristo ni lazima ufanane na wa Mungu au kulingana na mfano wa Muumba wake (Efe. 4:24; Kol. 1:10). Anatusisitiza "tuwe wafuasi wa Mungu" (Efe. 5:1). Yesu pia alisema kwamba Mungu ndiye kipimo cha maisha yetu: ***"basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu"*** (Mt. 5:48). ***"Basi iweni na huruma kama Baba yenu alivyo na huruma***" (Lk. 6:36). Petro alisema: ***"Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote. Kwa maana imeandikwa, mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu"*** (1Pet. 1:15-16). Kristo pia ni mfano kamili kwetu (Flp. 2:5; 1Pet. 2:21-24; 1Kor. 11:1). Kwa kuwa Mungu mwenyewe ndiye kipimo, lengo letu katika kujaribu kumfuata yeye ni lengo kuu. Ingawa hatutalifanya hili kikamilifu, lakini tutaishi vizuri zaidi kwa kujaribu kuwa wakamilifu na watakatifu kama Mungu. Lazima tutiwe moyo kwa nguvu na mfano wa Mungu kwa kufanya jitihada za kimaadili na za kiroho katika utakatifu na, kwa kuwa ukamilifu kwa nguvu za mwanadamu hauwezekani, utegemea zaidi na zaidi neema ya Mungu na kuendeleza upendo.

Neno moja la kuvutia la Kiyunani katika Agano Jipya kwa kawaida huwa linatafsiriwa "thamani." Linamaanisha "sambamba" au "kulinganishwa." Katika baadhi ya vifungu katika Agano Jipya tunahimizwa kuishi maisha yenye "thamani" ya kitu kingine. Hii ina

maana kwamba maisha yetu yanapaswa kuwa sambamba na, kulinganishwa na, au sawa na kitu kingine. Tunatakiwa kuishi maisha yenye thamani ya injili ya Kristo" (Flp. 1:27), "wajibu wetu kwa Mungu" (1The. 2:12), na wajibu wetu kwa Bwana, mkimpendeza kabisa" (Kol. 1:10). Tunapaswa kuishi maisha "yanayostahili wito wetu tulioitiwa" (Efe. 4:1). Wito wetu ni upi? Mungu hakutuita katika uchafu, bali katika utakatifu (1The. 4:7; linganisha na 1Tim. 4:9; Efe. 4:1). Ametuita "kutoka gizani na kutuleta katika nuru ya ajabu" (1 Pet. 2:9). Mungu anatuita "wana wa Mungu" (1Yoh. 3:1). Mungu ametuita "tuwe watakatifu" (Rum. 1:7; 1Kor. 1:2). Watakatifu si watu wachache walio wema ambao Papa amewatangaza kuwa watakatifu. Kila Mkristo ni mtakatifu. Tumetakaswa, yaani tumefanywa watakatifu, katika ubatizo (1Kor. 6;11; Efe. 5:25-27). Kwa kuwa Mungu anatuita tuwe watakatifu, imetupasa tuwe kama watakatifu.

Moyo wa maisha ya Mkristo ni upendo (1Kor. 13:1-3,13). Paulo aliandika: ***"Msiwiwe na mtu cho chote, isipokuwa kupendana; kwa maana ampendaye mwenzake ameitimiza sheria"*** (Rum. 13:8). ***"Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, umpende jirani yako kama nafsi yako"*** (Gal. 5:14; linganisha na Yak. 2:8; Mt. 22:36-40). Paulo anatupa maelezo ya kina ya namna ambavyo mtu mwenye upendo anafanya (1Kor. 13:7). Kristo mwenyewe ndiye kielelezo cha jinsi tunavyopaswa kupenda (Efe. 5:2, 25; 1Yoh. 3:23). Tunatakiwa kupenda "kama vile" anavyopenda (Yn. 13:34; 15:9-12). Sababu moja ya upendo kuwa wa muhimu katika maisha ya Mkristo ni kwamba tunatenda kwa nje kulingana na tulivyo ndani (Mt.12:33-35; 15:18-19; 23:25-26; Lk. 6:43-44). Ili tuwe wema kweli kweli, lazima tubadili mioyo yetu na mitazamo yetu (Rum. 12:1-2; Zab. 51:10; 119:36; 2Kor. 10:5; Efe. 4:22-23). Utu wetu wa ndani lazima uwe safi na wenye upendo ili matendo yetu ya nje yawe mema. Katika kuishi maisha ya Kikristo ni lazima tukwepe matendo ya nje ya dhambi na dhambi za ndani za moyo mwovu.

Sifa au wema mwingine chanya ni sehemu ya maisha ya Mkristo kama vile unyenyekevu, kutokuwa na ubinafsi, uvumilivu, kuwatendea wengine mema, kumwabudu Mungu, huruma, na tabia ya msamaha (Efe. 4:32). Andaa orodha ya sifa njema ambazo utajitahidi kuzifikia katika maisha yako kutoka katika vifungu vifuatavyo: Mt. 5:3-9; Gal. 5:22-23; Kol. 3:12-17; 1Tim. 6:11; Yak. 3:13, 17-18; 2Pet. 1:5-7. Utakapomaliza orodha ya sifa njema, tofautisha na sifa mbaya ambazo unapaswa kuzikwepa kulingana na vifungu vifuatavyo: Rum. 1:29-31; 1Kor. 6:9-10; Gal. 5:19-21; Kol. 3:5-10; 1Tim. 1:9-11; 2Tim. 3:2-5; Yak. 3:14-16; 1Pet. 2:1-2.

Njia nzuri zaidi ya kujifunza katika maisha ya Ukristo ni kusoma sehemu kubwa za Agano Jipya ambazo zinaelezea somo hili. Mafundisho mengi yametungwa takribani nusu ya pili ya kitabu cha Agano Jipya. Nusu ya sehemu ya kwanza ya mafundisho yanaelezea misingi ya kidini ambayo tunapaswa kuishi. Nusu ya sehemu ya pili inatuambia namna ambavyo imani yetu ya Kikristo inavyopaswa kutekelezwa katika maisha yetu (Tit. 2:1). Jifunze sehemu inayofuata ya vifungu vya Maandiko kuhusu namna ya kuishi maisha ya Kikristo. Biblia inafundisha kuhusu maisha ya familia, biashara, uhusiano wako na serikali, uadilifu binafsi, maadili ya ngono, na mambo mengine mengi zaidi (Mt. 5:1-7:28; 18:1-35; Rum. 12:1-4; Efe. 4:17-6:20; kol. 3;1-4; 1The. 4:1-12; Tit. 2:1-11; Ebr. 12:1-13:19; Yak. 1:2-5:20; 1Pet. 2:11-5:11). Kama Mkristo jizoeze “katika utauwa” (1 Tim. 4:7).

## Kanisa

Neno la Kiyunani la "kanisa" linamaanisha "kusanyiko, kukusanyika, mkutano, au kanisa". Unapofikiria kanisa, usichanganye na jengo. Kanisa linaweza kumiliki jengo na mali nyingine, lakini kanisa lina watu ambao wameokolewa na Yesu. Unapofikiria kanisa, usilichanganye na shirika la kanisa, uongozi, maaskofu, au muundo wa

madhehebu. Tena, kanisa linarejelea watu ambao wameokolewa, sio shirika au taasisi. Hata kabla ya Agano Jipya kuandikwa, Wayahudi walikuwa wametafsiri Maandiko ya Agano la Kale katika Kigiriki karibu karne mbili kabla ya Kristo kuzaliwa. Walitumia neno "kanisa" mara nyingi sana katika Agano la Kale lililotafsiriwa kwa Kiyunani, na hapo kimsingi lilirejelea watu wa Mungu, Israeli. Vivyo hivyo, katika Agano Jipya kanisa ni watu wa Mungu.

Neno "kanisa" linaweza kurejelea kanisa la ulimwengu wote ambalo lina Wakristo kote ulimwenguni. Hivi ndivyo Yesu alivyomaanisha aliposema: ***"Nitalijenga kanisa langu"*** (Mt. 16:18). Au "kanisa" linaweza kurejelea kusanyiko katika eneo moja kama vile kanisa la Korintho (1Kor. 1:2). "Kanisa" pia linaweza kutumika kwa Wakristo wanaokusanyika katika ibada (1 Kor. 11:18; 14:19). Kanisa lenyewe linaitwa kwa maneno mengi ya ufafanuzi katika Biblia. Hakuna jina moja lililotolewa katika Agano Jipya kwa kile ambacho kanisa linapaswa kuitwa. Jina la kusanyiko linaweza kutusaidia kulipata kwa kujumuisha jina la mji, mtaa, au eneo lingine. Njia hii ilitumika katika Agano Jipya inaporejelea "kanisa la Yerusalemu" au miji mingine (Mdo 8:1; 11:22; taz. Rum. 16:1; 1Kor. 1:2; 2Kor. 1:1) ; 1Thes. 1:1; 2Thes. 1:1), au ***"makanisa ya Galatia"*** ( Gal. 1:2; taz. Gal. 1:22; 1Thes. 2:14; 1Kor. 16:1, 19; Ufu. 1:4). Mahali palipofanywa mahususi sana kama vile "kanisa" linalokutana katika nyumba ya mtu fulani (Rum. 16:5; 1Kor. 16:19; Flp. 2).

Kanuni nyingine inaonekana dhahiri katika majina ya Agano Jipya kwa ajili ya kanisa kwa kuwa yanaelekea kumpa Mungu au Kristo utukufu, si binadamu fulani kama Petro, Paulo, Mariamu, Yohana n.k (1Kor. 1:10-17). Hivyo, kanisa linajulikana kama ***"nyumba ya Mungu"*** ( 1 Tim. 3:15 ), ***"kanisa la Mungu"*** au tena, ***"kanisa la Mungu"*** ( 1Kor. 1:2; 10:32; 11:16, 22; 15:9; 2Kor. 1:1; Gal. 1:13; 1Thes. 2:14; 2Thes. 1:4; 1Tim. 3:5; Mdo. 20:28), ***"kanisa la Mungu aliye hai"*** (1. Tim. 3:15 ), ***"makanisa ya Kristo"*** ( Rum. 16:16 ), au ***"kanisa lililo katika Mungu***

***Baba, na katika Bwana Yesu. Kristo"*** (1 Wathesalonike 1:1). Badala ya kutumia jina ambalo hukazia fundisho fulani la pekee au jina la mwanadamu, jambo bora zaidi ingekuwa kutumia majina yanayotoa utukufu na sifa kwa Mungu na Kristo. Zaidi ya yote, kanisa ni mali ya Mungu.

Asili ya kanisa inaonyeshwa katika tamathali nyingi zinazotumika kulielezea. Kanisa linalinganishwa na jengo au nyumba (1 Kor. 3:9; Ebr. 3:6; 1 Tim. 3:15). Kanisa ni "hekalu la Mungu," kwa sababu Mungu anakaa ndani ya Wakristo (1 Kor. 3:16-17; 6:19-20). Hekalu hili au jengo hili halikujengwa kwa matofali na mawe, bali kwa wanadamu ambao ni ***"mawe yaliyo hai"*** (1 Pet. 2:5). Kanisa ni ***"mwili wa Kristo,"*** na Kristo ndiye **"kichwa"** cha mwili ( Efe. 1:22-23; 4:4, 15-16; Kol. 1:18, 24 ). Ili kubadilisha sitiari kidogo, kanisa linafikiriwa kuwa ni mwili kwa kuwa kila mmoja wetu ana kipaji tofauti na tunategemeana sisi kwa sisi (Rum. 12:4-8; 1Kor. 12:14-26). Sitiari ya mwili inaangazia ushirika wetu kwa pamoja kama vile mifano ya familia kwa kanisa (Mt. 12:49-50; Efe. 2:19; 2Kor. 6:18; 1Tim. 5:1-2). Tunapaswa kushiriki pamoja na Wakristo wenzetu katika furaha na huzuni ( Rum. 12:15; 1Kor. 12:26; Gal. 6:2, 10 ). Kanisa ni "ushirika" katika maeneo mengi (Mdo. 2:42; 1Kor. 1:9; Gal. 2:9; Efe. 3:9; Flp. 3:10; 1Yoh. 1:3, 6-7) . Kanisa ni bibi-arusi wa Kristo, ambapo ina maana kwamba tunapaswa kuwa safi ili tuwe tayari kwa ajili ya siku moja tutakapoenda kuishi na Kristo mbinguni (Efe. 5:22-32; 2Kor. 11:2). Mtume Petro analielezea kanisa kwa uzuri akitumia hasa taswira ya Agano la Kale (1 Pet. 2:9-10):

> "Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema."

Utaratibu wa kanisa ni rahisi sana. Kristo ndiye mwenye mamlaka. Hili linadhihirika kutokana na sitiari mbalimbali anazotumiwa kuelezea uhusiano wake na kanisa. Yeye ndiye ***“mchungaji mkuu”*** ( 1 Pet. 5:4 ), ***“kichwa”*** ( Efe. 1:22-23; 4:4, 15-16; Kol. 1:18, 24 ), ***“jiwe la pembeni”*** ( Efe. 2:20 ), au ***“msingi”*** ( 1Kor. 3:11 ). Makusanyiko ya ndani ya kanisa katika siku za Agano Jipya yalisimamiwa na wazee ambao pia walijulikana kama maaskofu, wachungaji, au waangalizi ( 1 Tim. 3:1-7; Tit. 1:5-9; 1Pet. 5:1- ) 4; Flp. 1:1; Mdo. 20:28; Efe. 4:11; 1 Wathesalonike 5:12; Ebr. 13:17). Wazee walitunza kusanyiko ambapo walikuwa washirika. Hakukuwa na askofu au mzee ambaye alitawala makusanyiko kadhaa zaidi ya moja. Makusanyiko yote yalilazimika kumtii Kristo na mitume, lakini hakuna kusanyiko lililotawala kusanyiko lingine. Wazee walisaidiwa katika kazi zao na baadhi ya walioteuliwa kuwa mashemasi au watumishi wa kanisa (1 Tim. 3:8-13; Flp. 1:1). Pia, Kristo alitaka kanisa liwe na umoja. Umoja ni lengo ambalo ni la kutamanika kwa sababu huleta ufanisi katika kazi yetu na heshima katika jina la Bwana wetu (Yn. 13:34; 17:20-21; Rum. 12:16; 15:5; 1Kor. 1:10; 3:3; 2Kor. 13:11; Efe. 4:3; Flp. 2:2).

Je, unakuwaje mshirika wa kanisa? Ikiwa wewe ni muumini aliyebatizwa, umekuwa mshirika wa kanisa ulipobatizwa “katika” Kristo. Kwa kuwa kanisa ni “mwili wa Kristo,” basi uko kanisani kwa sababu wewe ni ‘Mkristo (Gal. 3:27; Rum. 6:3). Unapaswa, hata hivyo, kujihusisha na kusanyiko la waumini waaminifu. Unahitaji kuungwa mkono na kutiwa moyo na Wakristo wengine (Ebr. 3:13; 10:24-25). Ni vigumu kuishi maisha ya Kikristo ya upweke. Hiyo ni sababu moja kwa nini Yesu alikuja sio tu kuokoa watu mmoja mmoja, bali pia kujenga kanisa.

Baadhi ya makosa yanayohusiana na mafundisho ya kanisa yanapaswa kuzingatiwa. Ijapokuwa mtume Petro alisaidia sana kulianzisha kanisa baada ya kufufuka kwa Yesu, lakini hakupewa mamlaka ya kidunia juu ya kanisa. Petro alihubiri Injili na watu

waliokolewa (Matendo 2:14-47; 10:1-48). Pia aliandika nyaraka mbili za Agano Jipya na alihudumu kama mchungaji kwa waumini wengi wa karne ya kwanza (1 Pet. 5:1; Yoh. 21:15-17). Hata hivyo, haki na mapendeleo yoyote aliyopewa ( Mt. 16:17-19 ) yalitolewa pia kwa mitume wengine ( Mt. 18:1, 18; Yn. 20:23 ). Petro na mitume wote walikuwa sehemu ya msingi wa kanisa kwa maana ya kwamba wao ndio wahubiri wa kwanza na walikuwa mashahidi waliojionea ufufuo wa Yesu Kristo ( Efe. 2:20; 1Kor. 12:28; Ufu. 21:14 ) ), lakini kanisa limejengwa juu ya Yesu Kristo (Efe. 2:20; 1Pet. 2:6-8). Paulo aliandika: ***"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo"*** ( 1Kor. 3:11 ). Hakuna kitu kilichoandikwa katika Agano Jipya kuhusu Petro kutawala kanisa zima kama Papa, na hakuna kitu kilichoandikwa kuhusu warithi wa Petro katika nafasi yoyote kama hiyo. Petro mwenyewe alikataa kuabudiwa alipokuwa hai (Mdo. 10:25-26) na wakati fulani alionywa na wengine kwa makosa yake (Gal. 2:11-14). Hakuwa na mamlaka ya kusuluhisha mabishano peke yake (Matendo 15:1-30). Kwa hiyo, heshima, kuinuliwa, na mamlaka aliyopewa Petro na wanaodhaniwa kuwa waandamizi wake kama Mapapa huko Roma na Wakatoliki wa Kirumi ni tusi kwa cheo ambacho Kristo anapaswa kuwa nacho katika kanisa.

Kanisa linaundwa na ukuhani wa waamini wote (1 Pet. 2:9; Ufu. 1:6; 5:10). Kila Mkristo anaweza kukaribia kiti cha enzi cha Mungu Baba kwa maombi na ibada (Ebr. 10:19-22; Rum. 5:1-2; Efe. 2:18; 3:12; 1Yoh. 2:1-2) kupitia upatanishi wa Yesu Kristo, Kuhani wetu Mkuu ( 1 Tim. 2:5; Ebr. 2:14-18; 4:14-5:10; 7:1-10:39 ). Hatuhitaji kupitia mpatanishi au kuhani wa kibinadamu ili kupokea msamaha na wokovu kutoka kwa Mungu. Si lazima kwa mtu kwenda kwa padri kuungama dhambi. Kuungama dhambi kunaweza kufanywa kwa Mkristo yeyote na, muhimu zaidi, kuungama dhambi kunaweza kufanywa kwa Mungu katika maombi (Yak. 5:16; 1Yoh. 1:9). Zaidi ya hayo, hakuna

mwanadamu, ikimjumuisha kasisi wa Kikatoliki, aliye na haki ya kusamehe dhambi zetu. Hakuna anayesimama katika nafasi ya Mungu akiwa na nguvu ya wokovu na hukumu mikononi mwake. Tukiwa wanadamu tuna uwezo wa kufundisha kweli au kukataa ukweli, jambo ambalo linaweza kuathiri wokovu wa mtu ( Mdo. 13:38-39; Mt. 18:5-6, 18; 23:13; Lk. 11:52 ). Lakini Mungu ndiye mwamuzi wa mwisho anayesamehe au kuhukumu.

Kosa lingine ambalo watu wengi wa kidini hulifanya ni kumwabudu na kumtumikia Mariamu, mama yake Yesu. Mariamu alikuwa mwanamke mzuri wa Kiyahudi ambaye alichaguliwa kutoka "kati ya wanawake" kuwa mama wa Yesu Kristo (Lk. 1: 39-43), lakini Biblia inasema machache sana kuhusu maisha ya Mariamu. Wakati wa kifo cha Yesu aliwekwa chini ya uangalizi wa mtume Yohana (Yn. 19:25-27). Alimwamini Yesu kama walivyokuwa ndugu zake Yesu (Matendo 1:14). Katika Biblia hakuna mtu aliyewahi kuelekeza sala kwake. Hakuwa na nguvu za miujiza. Hakubaki bikira baada ya Yesu kuzaliwa (Mt. 1:24-25; 13:54-56; Mk. 6:3; Lk. 2:7). Alikuwa kielelezo kizuri cha mtu aliyejitiisha kwa Mungu kwa unyenyekevu na mtu aliyemwamini Yesu (Lk. 1:38), lakini hakuwa Mungu. Yeye si mwokozi wetu wala mpatanishi wetu, mtu hapaswi kuomba kwake. Nafasi aliyopewa Mariamu na Wakatoliki wa Roma inanyakua nafasi ambayo Yesu Kristo anapaswa kushikilia katika ibada yetu na ni tusi kwa ukuu wake (Kol. 1:15-20; Rum 8:34; 1Tim. 2:5; 1Yoh. 2) :1-2).

## Huduma na Uinjilisti

Kwa kuwa kanisa ni mwili wa Kristo, kazi ya kanisa ni kuendeleza utume wa Kristo ulimwenguni. Kama taifa la makuhani tunafanya kazi pamoja kumtumikia Mungu (Ebr. 9:14; 1Pet.2:5, 9). Ijapokuwa baadhi yao huwekwa rasmi kufanya kazi maalum, kama vile kuwa wazee, mashemasi, au walimu. Wakati huo huo, Wakristo wote wanapaswa

kuwa watumishi au wahudumu katika kazi ya Bwana ( Efe. 4:11-13; Mt. 20:26-28; 25:44, 45; Rum. 16:1-2). Kazi yetu ni kumtumikia Mungu na wanadamu. Utumishi wetu kwa Mungu katika ibada utazungumziwa katika sehemu inayofuata.

Hebu tuangalie kazi za kanisa zenye sehemu mbili kwa kanisa lenyewe na kwa ulimwengu. Kwanza, kanisa linapaswa kuwahudumia washirika wake lenyewe, kuwajenga, kuwasaidia kukua kiroho, na kuwasaidia kubaki na wokovu (Efe. 4:11-13; Kol. 1:28). Wengine ndani ya kanisa ni walimu au wahubiri ambao huwasaidia wengine kukua kiroho kwa kuwafundisha (Efe. 4:11; 1Tim. 4:11-16; 2Tim. 2:2; 3:10-4:5 ). . Wakristo wanapaswa kusaidia mahitaji ya kimwili ya Wakristo wengine (Mdo. 11:29; Gal. 6:10; 2Kor. 8:1-9:15; 1Yoh. 3:17-18 ). Katika kutumikiana tunafuata mfano wa Yesu (Mt. 20:28; Flp. 2:7-8). Wakristo wengi hufurahia ushirika pamoja na wengine na kuunda urafiki wa karibu ndani ya kanisa. Kama familia kanisa wakati mwingine inabidi liwaadhibu washirika wake lenyewe kwa matumaini ya kumleta mpotovu wa nidhamu kwenye toba na kuzuia dhambi isienee zaidi (1 Tim. 1:20; 1Kor. 5:1-13; Mt. 18). 15-17; 2Yoh. 10-11; 2Wathesalonike 3:14-15; Tit. 3:10-11).

Pili, kazi ya kanisa inaelekezwa kwa ulimwengu. Wakristo wanaishi katika ulimwengu lakini hawapaswi kuishi kama ulimwengu (Yn. 8:23; 15:19; 17:15-18), Kama vile mashua ndani ya bahari au ziwani inavyobaki kuelea maadamu haiingizi maji. Wakristo hawapaswi kushiriki dhambi za ulimwengu (2 Kor. 6:14-17). Maisha yetu yanapaswa kuwa nuru inayoangaza ulimwenguni, yakionyesha njia sahihi ya kuishi (Mt. 5:13-16; 1Pet. 2:12; 3:15-16; Flp. 2:15). Wakristo ni jeshi la Mungu katika ulimwengu huu katika vita dhidi ya uovu na dhambi (2 Kor. 10:3-5; Efe. 6:10-17). Hatutumii jeuri au njia za dhambi. Badala yake, tunatumia ushawishi, mfano mzuri, na kuhubiri ukweli ili kueneza Injili ulimwenguni (Mt. 28:19-20; 1Kor. 9:16). Kama vile Paulo alivyosema kwa ufasaha sana: ***“Lakini vyote pia vyatokana na***

***Mungu,..alitupa huduma ya upatanisho;..Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu"*** ( 2Kor. 5:18-20 ).

Ni maarufu sana kwa wasio Wakristo kudharau pindi kanisa linapokosea. Kwa kuwa kanisa linaundwa na wanadamu wanaokosea, wanaofanya makosa, kanisa lenyewe si kamilifu. Wakristo wanajua kwamba wao si wakamilifu, lakini pia wanajua kwamba Yesu Kristo ni mkamilifu. Yeye ndiye ambaye watu wanapaswa kumwangalia wanapohukumu Ukristo. Hata wakati mtu anapotazama makosa mengi ambayo Wakristo hufanya, tathmini ya haki ya ushahidi itaonyesha kwamba kanisa limefanya mema zaidi kuliko madhara kwa wakati wote. Madhara mengi yanayohusishwa na kanisa yalitokea kwa jina la Kristo, lakini yalifanywa na kanisa la uwongo au wasio Wakristo. Watu hawa walitumia jina la Kristo kama kinga kujaribu kutetea baadhi ya vitendo viovu. Waumini wa kweli wa Kristo wamefanya wema usioelezeka na usiopimika katika ulimwengu kupitia sala, ukarimu, kusaidia maadili ya familia, mafundisho, kazi za hisani, na matendo mengine mema. Kanisa linaundwa na watu bora zaidi ulimwenguni. Ingawa kila Mkristo na kusanyiko lina nafasi ya kuboreshwa, kanisa limekuwa kama mji juu ya mlima wenye mwanga wa kuwaongoza watu kwenda mbinguni (Mt. 5:14-16).

## Ibada

Kazi ya kanisa haielekezwi tu kwa ulimwengu, bali pia inaelekezwa kwa Mungu katika ibada. Ibada ni nini? Ibada inaweza kufafanuliwa kwa upana kama yote tunayofanya katika kumtumikia Mungu wetu (Warumi 12:1-2). Ukweli wa kujifunza kutokana na ufafanuzi huu ni kwamba maisha yetu yote yanapaswa kuishi kwa ajili ya Mungu (Kol. 3:17). Hatupaswi kutoa hata saa moja au mbili katika

juma katika kumwabudu Mungu na kisha kumsahau na kuishi kwa ajili yetu wenyewe katika siku zilizobaki. Kila kitu tunachofanya kinapaswa kufanywa kwa njia hiyo ili tuweze kumpendeza Mungu na kutii mapenzi yake. Lakini maana hii pana, na ya jumla kuhusu ibada sio lengo kuu katika sehemu hii. Ufafanuzi mdogo zaidi wa ibada ni "heshima na sifa zinazotolewa kwa Mungu." Kuabudu kunamletea Mungu thamani. Neno moja la Kiyunani ambalo mara nyingi hutafsiriwa "kuabudu" katika Agano Jipya humaanisha kuanguka chini na kuabudu, kusujudu, kuheshimu" (Mt. 2:2, 8, 11; 4 :9, 10; Yoh.4:23-24; 1Kor.14:25; Ufu.4:10; 5:14). Ibada ni kumsifu na kumheshimu Mungu kwa utukufu wake mkuu. Jifunze mazingira ambayo yapo mbingunimbele ya kiti cha enzi cha Mungu ili kupata ufahamu wa kile ambacho ibada inahusisha ( Ufu. 4:1-5:14; Isa. 6:1-5; 56:7; Mt. 21:13). Lakini usimfikirie Mungu kuwa ni Mungu mbinafsi asiye na kitu na anataka tumsifu kila wakati ili kujenga utu wake (Mdo. 17:24-25; Zab. 50:10-12) Mungu ametuamuru tumwabudu, kwa sababu ni kwa faida yetu. .Tunahitaji ibada ili kutimiza asili yetu kama viumbe vya kiroho. Katika kumwabudu Mungu tunawatia moyo wengine na kujisaidia wenyewe.

Kwa sababu Mungu yuko kila mahali, ibada ya Kikristo inaweza kufanywa popote. Si lazima mtu awe katika mahali patakatifu au jengo fulani ili kumwabudu Mungu (Yn. 4:19-24). Watu wanaweza kuabudu katika majengo ya kukodi, katika nyumba, nje katika mazingira ya kiasili, au katika majengo yanayomilikiwa na kusanyiko ( Rom. 16:5; 1Kor. 16:19; Kol. 4:15; Mdo. 2:46; 5:42; 16 ) :13; 20:7-8). Ibada ya Kikristo haiamuliwi na mavazi rasmi ya nje, bali kwa kububujika kwa ndani yale tunayohisi mioyoni mwetu kwa Mungu. Hii ndiyo sababu maisha safi na moyo wa unyoofu ni matokeo muhimu katika ibada inayokubalika (Zab. 15:1-5; 24:3-4; Mt. 5:8). Mungu ni Roho, kwa hiyo, ibada yetu lazima itiririke kutoka mioyoni mwetu. Yesu alisema hivi: ***"Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu***

***katika roho na kweli"*** (Yn. 4:24). Ikiwa wewe ni Mkristo na huwezi kupata kanisa karibu nawe ambalo ni aminifu katika kweli, basi unaweza kumwabudu Mungu nyumbani kwako pamoja na familia na marafiki.

Kanisa la kwanza lilikusanyika siku ya kwanza ya juma, Jumapili, ili kuabudu (Matendo 20:5-7; 1Kor 16:1-2). Wayahudi waliabudu siku ya saba ya juma, Jumamosi au Sabato, lakini Wakristo hawakuendeleza desturi hiyo. Kwa sababu Yesu alikuwa amefufuliwa siku ya kwanza ya juma, siku hiyo ilijulikana kama siku ya Bwana na ilikuwa ni siku ya Wakristo kukusanyika kwa ajili ya ibada (Ufu. 1:10; Mt. 28:1; Mk. 16:1 ) 2). Bila shaka, hakuna ubaya kwa Wakristo kufanya matendo mengine ya ibada siku yoyote na wakati wowote isipokuwa moja tu ambalo ni kushiriki Chakula cha Bwana, kwani kitendo hiki hufanywa katika siku ya kwanza tu. Itakusaidia kukua kiroho ikiwa unatenga muda peke yako wiki nzima kusoma Biblia yako na kumwomba Mungu (Mt. 6:6). Wakristo wengi hufurahia kukusanyika katika nyumba au mahali pengine juma nzima ili kuimba nyimbo za Kikristo, kusali kwa Mungu, kujifunza Biblia, na kufaidika na ushirika mzuri wa Kikristo (Matendo 2:46; 5:42). Kutana na Wakristo wengine mara nyingi unavyotaka, lakini hakikisha unakuza tabia ya kukusanyika pamoja na Wakristo wengine kila Jumapili ili kuabudu, isipokuwa kama umezuiwa kufanya hivyo kwa sababu ya kizuizi kama vile ugonjwa (Ebr. 10:25). Unahitaji kutiwa moyo mara kwa mara na usaidizi unaotokana na ibada na ushirika na waumini wengine.

Sio kila kitu ambacho Wakristo hufanya wakati wa kusanyiko la Jumapili ni ibada kwa maana kamili ya kuonyesha heshima kwa Mungu. Kusudi lingine la kusanyiko ni kutiana moyo na kufundishana ( 1 Tim. 4:13; 1Kor. 14:19, 26 ). Wakristo wanaimba katika ibada. Baadhi ya nyimbo zinapaswa kuwa ni nyimbo za sifa na ibada kwa Mungu na Kristo, lakini nyimbo nyingine zinaweza kuwa ni nyimbo ambazo kwazo tunafundishana na kutiana moyo ( Efe. 5:19-20; Kol. 3:16; Mdo. 16:25;

1Kor 14:15). Usomaji wa Biblia ni kipengele cha kawaida cha ibada ya Kikristo ambacho katika hicho manufaa mengi yanaweza kupatikana (Ufu. 1:3; 1Tim. 4:13; 1The. 5:27). Mafundisho, kutia moyo, na maagizo yanayotegemea Biblia, ni mambo mengine ya kawaida katika ibada ya Kikristo na ni muhimu sana kwa ukuaji wa Kikristo (1 Tim. 4:13-16; 5:17; 2Tim. 2:1-2; 3:10 ; 16; Matendo 20:20-21; Yak. 3:1). Kukusanyika pia ni wakati wa ushirika, wakati wa kuwa pamoja na Wakristo wengine, na kushiriki pamoja ibada yetu ya pamoja (Rum. 12:3-8, 15; 16:16; 1Kor. 16:20; 1Yoh. 1:3-4).

Kanisa kwa kawaida huwa na hazina ambayo hutumika kwa kazi ya ukarimu, kusaidia viongozi wake, na kwa ajili ya kujitolea mahitaji mengine ( Rum. 12:13; 15:25-27; 1Kor. 9:1-14; 2Kor. 8:1-9:15; Ebr. 13:1-3; 1Tim. 5:3-18; Yak. 1:27). Jumapili ni wakati mwafaka kwa Wakristo kutoa kwenye hazina ya kanisa (1Kor. 16:2). Kwa kufanya hivyo tunaonyesha umoja na ushirika wetu sisi kwa sisi. Kwa kweli, neno la Kiyunani la "ushirika, uhusiano wa karibu" linatumika katika kurejelea kuchangia kazi ya kanisa ambayo ni "ukarimu, ushiriki" kama "ishara ya ushirika au uthibitisho wa umoja wa udugu" (2Kor. 8:4; 9:13; Rum. 15:26; Ebr. 13:16). Wayahudi walikuwa na utaratibu wa kutoa zaka, yaani, kutoa asilimia kumi. Wakristo wana mfumo rahisi zaidi wa kutoa kama mtu amefanikiwa na kama inavyohitajika (1Kor. 16:1-2).

Maombi ni aina muhimu ya ibada ya umma na ya faragha. Wakristo wanaamini kwamba Mungu yuko, kwamba anasikia sala, kwamba anawapenda wanadamu, na kwamba anajibu sala. Siku zote Mungu hatupi kile tunachoomba, hususani pale inapokuwa kutokuwa na manufaa kwetu, lakini tunaweza kuwa na hakika kwamba Mungu yuko tayari kutupatia kile kilicho bora zaidi kwa ajili ya ustawi wetu wa kiroho ( Rum. 8:28 ). Kila mtu anapaswa kusitawisha tabia ya kuomba mara kwa mara (1 The. 5:17; Rum. 12:12; Kol. 4:2; Lk. 18:1). Epuka mambo ambayo yatazuia maisha yako ya maombi, kama vile shida nyumbani ( 1 Pet. 3:7 ), roho ya kutosamehe ( Mt. 6:14-15; Efe. 4:32 ),

kutokuwa na unyoofu, ukosefu wa toba ( Zab. 66:18; Isa. 1:15), dhambi isiyoungamwa ( 1 Pet. 3:12 ), au ukosefu wa imani katika Mungu ( Yak. 1:6-8 ). Kwa upande mwingine, kuna mambo mengi yatakayosaidia maisha yako ya maombi, kama vile maisha bora ya kimaadili (Zab. 24:3-4), roho ya utii (1 Yoh. 3:21-22), tabia ya uchaji (Mt. 6:9) ), unyenyekevu, kumwamini Mungu ( Mt. 21:22; Mk. 11:24 ), unyoofu ( Mt. 6:5-6; Zab. 17:1 ), na moyo wenye shukrani ( Kol. 4:2; Flp. 4:6). Bwana wetu alikuwa kielelezo bora cha mtu aliyesali ( Yn. 17:1-26; Mt. 14:23; 26:36; Lk. 5:16; 6:12; 9:28 ), naye alifundisha mengi kuhusu sala ( Yoh. Lk. 11:5-13; 18:1-8), kama walivyofanya wengine (1 The. 5:16-25; 1Tim. 2:1-8; Yak. 5:13-18 ). Wanafunzi walimwomba Yesu awafundishe jinsi ya kuomba, na mafunzo yalikuwa ni kielelezo kamilifu ambacho kinaeleza mambo yote makuu ambayo mtu anapaswa kushughulikia katika maombi:

> "Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. [Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.]" (Mt. 6:9-13; taz. Lk. 11:1-4).

Meza ya Bwana au ushirika ni ibada ya ukumbusho inayomheshimu Yesu Kristo. Ilianzishwa na Yesu alipoadhimisha mlo wake wa mwisho wa Pasaka pamoja na wanafunzi (Mt. 26:17-30; Mk. 14:22-24; Lk. 22:14-23; 1Kor. 11:23-26). Aliwaagiza wafuasi wake: ***"Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" (*** 1Kor. 11:24-25 ). Kusudi la Chakula cha Bwana ni kutukumbusha kifo na ufufuo wa Yesu (1 Kor. 11: 24-26). Meza ya Bwana haipaswi kufanywa kuwa karamu kwa kusudi la kujaza matumbo yetu (1 Kor. 11:34). Kusudi lake ni

kutafakari, kujichunguza, na kuabudu (1Kor. 11:27-28). Ni wakati wa ushirika ambapo tunaweza kuonyesha umoja na waamini wengine (1Kor. 10:16-17; 11:29-33). Mkate na mzao wa mzabibu ni ishara ya kutukumbusha mwili na damu ya Bwana wetu. Mkate usiotiwa chachu, yaani, mkate usio na amila, ndio unaopaswa kutumiwa, kwa sababu chachu ni mfano wa dhambi. Bwana wetu hakuwa na dhambi kama dhabihu yetu kamilifu, mkate usiotiwa chachu unatukumbusha yeye kama mwana-kondoo asiye na dosari (1 Kor. 5:7; Mk. 14:1). Hii inafanya Chakula cha Bwana kuwa wakati mzuri kwa sisi kufanya upya ahadi yetu ya kujaribu kushinda dhambi katika maisha yetu (1 Kor. 11: 27-32). Mzao wa mzabibu ni maji ya zabibu ambayo, kwa rangi na umbile lake, hutukumbusha damu ambayo Yesu alimwaga kwa ajili ya dhambi zetu. Wakristo wanapaswa kushiriki karamu ya Bwana kila siku ya kwanza ya juma kama onesho la umoja wa kanisa linalokusanyika kila Jumapili (1 Kor. 10; 16-17), kama ukumbusho kwamba Yesu yu hai na yuko kwa sababu alifufuka ( 1Kor. 11:26 ), kwa sababu ni siku ya Bwana, na kwa kuiga desturi ya kanisa la kwanza ( Mdo. 20:5-7; 1Kor. 16:1-2 ).

Maadhimisho ya Chakula cha Bwana kwa Wakatoliki yanaitwa Misa, inahusishwa na fundisho la uwongo la badiliko la mkate kuwa mwili, na divai kuwa damu. Wanaamini kwamba mkate na mzao wa mzabibu vinabadilishwa kuwa mwili na damu ya Yesu na kwamba anatolewa dhabihu tena wakati wa maadhimisho hayo. Agano Jipya linafundisha kwamba mateso na kifo cha Yesu vilikuwa tukio la wakati mmoja tu lililowatosheleza wanadamu wote (Ebr. 7:27; 9:12, 24-28; 10:10-14; Rum. 6:9). . Yesu hatolewi tena na tena. Yesu aliposema hivi kuhusu mkate: ***"Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu,"*** na kuhusu kikombe: ***"Nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu"*** (Mt. 26:26-28) alikuwa akizungumza kwa mafumbo. Kwa uwazi hakumaanisha kwamba ulikuwa ni mwili wake halisi au damu yake halisi, kwa sababu alikuwa ameshika mkate na kikombe mikononi

mwake. Hii ni tamathali kama ilivyokuwa kauli nyingi zinazofanana na hizo za Yesu (Yn. 10:7, 14; 15:5; Mt. 5:13-14). Badala ya badiliko, Wakristo wanaamini kwamba Yesu yuko kiroho wakati kanisa linapokusanyika katika ibada (Mt. 18:20). Mkate na kikombe ni ukumbusho wa mfano wa uwepo wake na wa mwili na damu aliyotoa kwa ajili ya dhambi zetu juu ya msalaba wa Kalvari.

Agano Jipya halitoi utaratibu ambao kwa huo huduma za ibada zinapaswa kuendeshwa. Wanaume wamepewa jukumu la uongozi katika makusanyiko ya ibada, kama walivyo nyumbani na kanisani pia (Mwanzo 1:26-27; 2:18; 3:16; 4:7; 1Kor. 11). 2-16; 14:33b-36; Gal. 3:28; Efe 5:21-33; Kol. 3:18-19; 1Tim. 2:1-15; 3:1-13; 1Pet. 3: 1-7). Ibada inapaswa kufanywa kwa mtazamo sahihi, kwa utaratibu, na kulingana na kweli au Maandiko (Yn. 4:24; 1Kor. 14:40). Ibada inayofanana na ifuatayo ingempendeza Mungu kama ingefanywa kwa njia ya uchaji. Unapokusanyika pamoja na Wakristo wengine, unaweza kuanza kwa kumwomba Mungu. Hii inaweza kufuatiwa na kuimba na sala zaidi. Mtu anaweza kusoma fungu la Maandiko ili wote wasikie. Ikiwa mtu ana sifa za kustahili kufundisha, katika mfumo wa mahubiri ni jambo zuri. Meza ya Bwana inapaswa kuadhimishwa wakati fulani na inaweza kuandamana na sala na nyimbo zaidi. Kukusanyika ni wakati mwafaka wa kuchukua changizo itakayotumika kuwasaidia wahitaji au kufadhili kazi nyingine za kanisa. Matangazo ya taarifa muhimu yanaweza kufanywa na kila mtu. Kwa mfano, mtu anaweza kuwaona wagonjwa na kuwaombea. Ibada inaweza kufungwa kwa maombi au wimbo. Sala, kuimba, kusoma Biblia, kufundisha, Meza ya Bwana, na changizo ni njia za kimapokeo ambazo kwazo Wakristo wamekuwa wakiendesha makusanyiko yao siku zote.

# Wakati Ujao

Mtazamo wa Kikristo wa historia ni kwamba ulimwengu huu ulikuwa na mwanzo, ambao tunauita Uumbaji (Mwa. 1), na utakuwa na mwisho ambao utatokea katika ujio wa pili wa Kristo, kila mtu lazima asimame mbele ya Mungu na Kristo katika hukumu. Katika hukumu hiyo kila mtu atapelekwa ama mbinguni au Jehanum milele. Mungu ni mwenye enzi na anafanya mapenzi yake katika historia, na lengo la mambo yote katika ulimwengu huu ni utukufu kamili wa Yesu Kristo kama Bwana (Flp. 2:9-11; Kol. 1:16). Uzima hutoka kwa Mungu, na tumaini la uzima wa milele liko ndani yake kikamilifu (1 Tim. 6:16). Je, unaingia wapi katika mpango huu waMungu?Ni vema ukafanya uchaguzi mzuri kwa ajili ya siku zijazo kwa hatima yako (Zab. 90:12; Yak. 4:14; Mt. 16:26).

Kwa kuwa sisi ni wanadamu, sote lazima tukabili kifo siku moja. Biblia haifundishi kuzaliwa upya katika mwili mwingine au kuhama kwa nafsi katika mfululizo wa kuzaliwa, maisha, na vifo. Tutakufa mara moja tu (Ebr. 9:27). Sisi miili ya kufa; lakini, kwa sababu sisi ni viumbe vya kiroho, sehemu yetu huendelea kuishi hata baada ya kifo (2 Kor. 5:12; 2 Pet. 1:13-14). Kifo kinafafanuliwa katika mtazamo wa kiroho kuwa mahali ambapo nafsi au roho inauacha mwili (Yak. 2:26). Kwa kawaida tunaogopa kifo, lakini injili inatupa tumaini na inaweza kutusaidia kushinda hofu hii (Zab. 39:5; Rum. 7:24; Ebr. 2:15; 1 Kor. 15:26; Flp. 1:21-23). Maandiko ya Agano la Kale hayasemi mengi kuhusu maisha baada ya kifo. Aliachiwa Yesu na maandiko ya Agano Jipya kulielezea hili kikamilifu zaidi. Paulo alisema kwamba Yesu Kristo, "***aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili***" (2 Tim. 1:10). Na ni kwa njia ya Yesu Kristo uchungu wa mauti na dhambi, vinaweza kuondolewa, huku akitupatia ushindi juu ya mauti (1 Kor. 15:54-57).

Je, hali ya roho inakuwaje hapo katikati.yaani baada ya kifo na siku ya hukumu? Hali hii inaitwa hali ya katikati. Watu wengine wanafikiri kwamba roho hulala wakati huu na itaamshwa katika ujio wa pili wa Yesu Kristo. Biblia inatumia neno "usingizi" kufafanua mtu aliyekufa, lakini hayani maelezo tu ya jinsi mwili wa mtu aliyekufa unavyoonekana kwa wale walio hai (1 The. 4:13). Mtu anakuwa amelala kwa kuwa hawezi kufanya kazi tena katika ulimwengu huu wa mwili (Ufu. 14:13). Vifungu vingine vya maandiko vinadokeza kwamba roho za wale waliokufa zina ufahamu baada ya kifo (2 Kor. 5:8; Lk. 16:19-31). Nafsi au roho za wale waliokufa huenda kuzimu. Kuzimu kumegawanyika katika sehemu mbili (Lk. 16:26). Sehemu nzuri inaitwa Paradiso, na hii ndiyo hali ya wale waliookolewa (Lk. 23:39-43; Mdo. 2:27). Sehemu mbaya inaitwa matesoni, na hii ndiyo hali ya wale waliopotea (Lk. 16:23). Hatima yetu ya milele inatiwa muhuri wakati wa kufa. Maandiko hayaonyeshi habari zozote kuhusu nafasi ya pili baada ya kifo. Vivyo hivyo maandiko hayasemi chochote kuhusu toharani au moto wa adhabu ambao wakristo wengi wanapaswakuvumilia ili kutakaswa kabla ya kwenda mbinguni. Ikiwa wewe niMkristo mwaminifu unapokufa, upatanisho wa Yesu Kristo unalipia dhambi zako zote (1 Yoh. 1:6-10). Mafundisho ya Kikatoliki ya Rumi kuhusu toharani kwa makosa yanaweka kikomo juu ya msamaha wa Mungu unaopatikana kupitia damu ya Yesu.

Mwisho wa dunia hii utatokea katika ujio wa pili wa Yesu Kristo. Hakuna anayejua ni lini ujio wa pili utatokea (Mt. 24:44). Yesu mwenyewe alisema kwamba hajuini lini itatokea, ila Baba peke yake (Mt. 24:36). Jihadharini na wale wanaopanga tarehe na kutoa madai kwamba wanaweza kusoma ishara na kujua wakati ujio wa pili utakapotokea. Mungu ameahidi kwamba Yesu atarudi, na Mungu hutimiza ahadi zake daima. Ingawa watu wengine wana shaka, tunapaswa kuendelea katika imani. Wengine watajaribu kumfanya

Mungu afuate ratiba ya wanadamu, lakini Mungu atatenda kulingana na mapenzi yake mwenyewe (2 Pet. 3:1-14). Kwa sababu hatujui Yesu atarudi lini, tunapaswa kuwa tayari kila wakati (Mt. 24:44). Fundisho la kuja mara ya pilina mwisho wa dunia lituchochee kuishi maisha matakatifu. Kama Petro anavyoeleza, "***Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa***" (2 Pet. 3:11). Kwa sababu ujio wa pili wa Yesu Kristo unamaanisha wokovu na makao mbinguni kwa wakristo, unaelezewa kama, "***tumaini letu lenye baraka***" (Tit. 2:13).

Yesu atakaporudi katika ulimwengu huu, kutakuwa na ufufuo wa jumla wa wanadamu wote. Yesu alisema, "***kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu***" (Yn. 5:28-29). Wale waliokufa watafufuliwa, na wale ambao wangali hai wakati wa kuja mara ya pili kwa Kristo wataungana nao kwa ajili ya siku ya hukumu, na kisha kuingia katika umilele (1 The. 4:13-18). Wakati roho au nafsi zetu zinapounganishwa tena na miili yetu katika ufufuo, mabadiliko yatatokea. Tutapokea mwili mpya wa ufufuo ambao hautakufa kamwe (1 Kor. 15:35-59). Hatujui hali halisi ya uwepo huu mpya, lakini tunajua utakuwa kama mwili wa ufufuo wa Yesu (1 Yoh. 3:2).

Mara baada ya ujio wa pili wa Kristo na mwisho wa dunia, kutakuwa na hukumu ya jumla ya wanadamu wote. Tutahukumiwa na Mungu na Kristo (Yn. 5:22-27; Mdo. 17:30-31; Rum. 14:10; 2 Kor. 5:10; 2 Tim. 4:1; Ebr. 12:23). Mungu atatuhukumu kulingana na mambo tuliyoyafanya katika maisha haya kwa kiwango cha Neno lake (Ufu. 20:12; Yn. 12:48; Rum. 2:6,16). Kutakuwa na mgawanyiko mkuu wa wanadamu kati ya wale waliookolewa na wale waliopotea(Mt. 25:31-

46). Waliookoka wataambiwa, "***Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu***" (Mt. 25:34). Waliopotea wataambiwa, "***Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake***" (Mt. 25:41). Siku ya hukumu si tukio la kutisha kwa muumini wa Kristo, kwani tutapewa tuzo siku hiyo badala ya kuhukumiwa (Rum. 8:1; Mk. 9:41; Lk. 6:35).

"Mbingu" ni jina ambalo wakristo wanalitumia kurejelea hali ya furaha ya milele ambayo Mungu atawapa watoto wake. Mbingunimahali pazuri sana kiasi kwamba lugha na fikra za mwanadamu ni vigumu kupambanua. Hivyo, mara nyingi Biblia inatumia lugha ya alama na mfano kuielezea mbingu (Ufu. 21:1-22:5). Mbinguni ni mahali pazurisana, maana tutakuwa pamoja na Bwana Yesu Kristo (Yoh. 14:13; Flp. 1:23; 1 The. 4:16-17). Ni kama kuwa kwenye sikukuu au karamu kuu (Mt. 22:1-14; Ufu. 19:9). Mtume Yohana aliona maono haya kuhusu Mbinguni, maana alisema,

> "Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita" (Ufu. 21:3-4).
>
> "Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo, katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila

> mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa. Wala hapatakuwa na laana yo yote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia; nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele" (Ufu. 22:1-5).

"Jehanum" ni neno ambalo Wakristo wanalitumia kuelezea hali ya upotevu wa milele kwa wale wote ambao si waaminifu kwa Yesu Kristo. Neno "jehanamu" hapo awali lilirejelea dampo la taka nje ya mji wa Yerusalemu. Palikuwa na mahali ambapo takataka zilitupwa na ziliendelea kuwaka daima, mahali pa moshi, moto, uchafu, uvundo, na ufisadi. Ni picha ya kutukumbusha sisi kwamba hatutaki kwenda Jehanumu. Maelezo ya Biblia kuhusu kuzimu mara nyingi ni ya kitamathali kisitiari, yaani lugha ya alama na mfano, kama yalivyo upande wa mbinguni. Jehanamuni mahali pa giza, kwa sababu panamaanisha kutengwa na Mungu (Mt. 25:30; 2 Pet. 2:4; Yud. 13). Ni mahali pa moshi na moto (Mt. 13:42; 25:41; Mk. 9:48; Ufu. 20:10-15) na maumivu (Mt. 25:30; Ufu. 14:11). Mtu akishahukumiwa kwenda jehanum,hakuna namna ya kutoka. Hasara ni ya kudumu na hakuna matumaini (Mt. 25:10,46; Ufu. 14:11). Ni rahisi kuona kwa nini Yesu aliwaonya watu kuhusu jehanamu (Lk. 12:4-5; 13:28; Mt. 5:29-30; 10:28).

Jihadhari na mafundisho fulani kama vile imani ya kabla ya milenia au kipindi cha utawala [miaka 1,000 ya utawala wa Kristo duniani kabla ya kwenda mbinguni]. Watetezi wa mafundisho haya mara kwa mara huweka tarehe za ujio wa pili wa Kristo au mwisho wa dunia. Wanazungumza juu ya unyakuo na utawala wa milenia wa Kristo duniani, lakini hakutakuwa na unyakuo wa siri watakatifu

watakapotoweka ghafla. Wala hakutakuwa na kurudi kwa Kristo kutawala duniani kwa miaka 1,000. Kristo atakaporudi, kila mtu atafufuliwa na siku ya hapo hukumu na umilele vitafuata, wala sio utawala wa kidunia wa Kristo (Yn. 5:28-29; 1 The. 4:13-17; Ebr. 9:28; Ufu. 1:7; 1 Kor. 15:23-24).

Watu hao wenye imani ya kabla ya milenia hufanya makosa mawili makubwa katika kutafsiri Biblia. Kwanza, wanafikiri juu ya ufalme wa Mungu na utawala wa Yesu kama utawala wa vitu vya kimwili katika ulimwengu huu. Lakini ufalme wa Yesu upo sasa kama utawala wa kiroho (Yn. 18:36; Rum. 14:17). Yesu tayari ni mfalme wa wafalme na ufalme wa Mungu upo tayari (Mt. 3:2; 11:12; 12:26-28; Mk. 9:1; Lk. 1:32-33; 16:16; Mdo. 2:29-33; 7:56; Efe. 1:20; Kol. 1:13; Ebr. 2:9; 12:28; Ufu. 1:6,9; 11:15).Pili, wanachukua vifungu vingi vya maandiko ambavyo tayari vimetimizwa na kudai kuwa bado havijatimizwa katika matukio ya siku hizi huko Palestina. Vifungu vingi ambavyo wanavielekezea fikira zao tayari vimetimizwa ama katika kurudi kwa Israeli kutoka utumwani Babeli au katika maangamizi ya Yerusalemu yaliyotekelezwa na Warumi mwaka wa70 B.K.(Mt. 24:1-28; Mk. 13:1-23; Lk. 21:5-36). Madai yao daima kitabu cha Ufunuo kinatabiri matukio ambayo bado hayajatokea, lakini kiukweli karibu ufunuo wote tayari umetimia. Maana mada yake kuu ni mateso ya kanisa la awaliyaliyofanywa na utawala wa kirumi (Ufu. 17:12; 15:18), Kwa sababu wakristo hawakuabudu sanamu au mtawala wa kirumi (Ufu. 1:9; 2:10,13; 6:9-11; 7:9,13-14; 9:20-21; 12:17; 13:5-6, 15-17; 14:9-13; 16:2,5-6; 17:6; 18:24; 19:2,20; 20:4).

## Utatu Mtakatifu

Neno "Utatu" halitumiki katika Biblia, lakini mara nyingi linatumiwa na Wakristo kuelezea uelewa wao wa mafundisho ya Mungu. Wakristo ni waamini Mungu mmoja, yaani, wanaamini kuwa

kuna Mungu wa kweli mmoja tu. Kuna watu duniani wanaamini kwamba kuna miungu kadhaa, hata maelfu, hata mamilioani. Lakini Wakristo, panoja na wayahudi, wanaamini katika Mungu mmoja tu (Kum. 6:4; Mk. 12:29; 1 Kor. 8:4; Yak. 2:19).Tunamjua Mungu huyu mmoja kwa njia tatu, kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Kuna tofauti kati ya hawa watatu; hata hivyo, pia kuna umoja kati yao. Tayari tumejifunza kwamba Yesu Kristo ni Mungu, yaani katika Uungu hasa (Yn. 1:1; 20:28; Flp 2:6). Kwa sababu Yeye ni Mungu, anastahili ibada yetu (Ufu. 5:1-14). Basi ujue kwamba ndivyo ilivyo kwa Baba na Roho Mtakatifu.

Baba ni Mungu, yaani asili ya Uungu (1 Kor. 8:6; Gal. 1:1; Efe. 4:6; 1 Pet. 1:2; Yn. 6:27). Neno "Mungu" linapotumiwa katika Biblia bila ufafanuzi wowote zaidi, mara nyingi sanalinatumika kumrejelea Baba. Mungu ni mkuu katika hali na tabia yake. Zifuatazo ni baadhi tu ya sifa za Mungu Baba. Anajitegemea (Isa. 40:13; Zab. 50:12; Mdo. 17:25), ni wa milele (Zab. 90:2-4; Kum. 32:40; Yak. 1:17), ni Roho (Yn. 4:24; Kum. 4:15; Mdo. 17:29), ni mweza wa yote (Isa. 14:27; Zab. 2:4), anajua yote (Zab. 147:5), yupo kila mahali (Yer. 23:23-24; Zab. 139:7-12), Mungu Baba ni mwenye upendo (1 Yoh. 4:8; Zab. 118:1-29; Rum. 8:35-39), Ni Mtakatifu (Isa. 6:3-5; Zab. 99:9; Ufu. 15:4), ni mwenye rehema (Kum. 4:31; Zab. 145:8), ni mwenye haki (Isa. 5:16; Zab. 11:7). Mungu ni mkuu, anatisha, na anastahili sana kuabudiwa na sisi (Ufu. 4:1-11; Mt. 4:10; Lk. 4:8; Kum. 6:13).

Roho Mtakatifu pia ni Mungu, katika hali ya Uungu. Angalia katika Matendo 5:34 kwamba Anania alimdanganya "Roho Mtakatifu," hivyo alimdanganya "Mungu" (ling. 1 Kor. 3:16-17; 6:19-20). Hiyo ni kwa sababu Roho Mtakatifu ni Mungu. Roho Mtakatifu anazo sifa za Mungu (Rum. 8:2; Yn. 16:13; Ebr. 9:14; Zab. 139:7), anafanya kazi ambazo ni Mungu pekee awezaye kufanya (Mwa. 1:2; Zab. 104:30; Yn. 3:8; 16:8; Rum. 8:11; 2 Pet. 1:21), anafanywa kuwa sawa na Mungu

(Mt. 28:19; 2 Kor. 13:13)na anapokea utukufu na kuabudiwa, ambapo Mwenyekustahili ni Mungu tu (1 Kor. 3:16). Usimtaje Roho Mtakatifu kama "kitu" kana kwamba Roho Mtakatifu ni nguvu Fulani, siyo nafsi hai yenye utashi. Roho Mtakatifu ni nafsi hai na anaweza kudanganywa au kuhuzunishwa (Mdo. 5:3-4; Efe. 4:30). Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Wakristo ili kututakasa na kututia nguvu (Mdo. 2:38; 5:32; Rum. 8:9-16,26; 1 Kor. 3:16-17; 6:11, 19-20; 12:13; 2 Kor. 1:22; 5:5; Gal. 4:6; Efe. 1:13; 3:14-16; Tit. 3:5; 1 Yoh. 4:13; Yud. 19). Roho Mtakatifu humshuhudia Yesu Kristo na hutuombea (Rum. 8:26-27).

Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, basi wote ni Mungu, wote kila mmoja ni sawa na mwingine, na wameungana kuwa mmoja (Yn. 10:30; 15:26; Mt. 28:19; 1 Pet. 1:2; 1 Kor. 12:4-6). Angalia jinsi Paulo anavyowazungumzia katika hali ya umoja, "***Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote***" (2 Kor. 13:14). Fundisho la utatu halijumuishi misimamo miwili mikali ya Mungu mmoja na miungu wengi. Wakristo hawaamini kwamba Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wote ni wale wale bila tofauti kati yao. Lakini, kwa upande mwingine, Wakristo hawaamini kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni miungu watatu tofauti. Je, kuna nafasi yoyote kati ya mambo haya mawili ya kupita kiasi kwa Mungu ambaye ni mmoja na bado watatu? Sisi kama viumbe wenye ukomo wa kufikiri na kutenda kazi ndani ya mipaka ya akili ya kibinadamu, hatuwezi kutarajia kumwelewa Mungu kikamilifu. Mungu hana mwisho. Kumfahamu Mungu kikamilifuni zaidi ya uwezo wetu. Kipengele cha siri kimebakia katika fundisho la utatu hata baada ya wasomi wakuu wa ulimwengu kujaribu kukielewa katika kipindi cha miaka 2000 iliyopita. Tunachoweza kusema ni kwamba tunamjua Mungu mmoja kuwa Baba, Mwana na Roho Roho Mtakatifu.

## Roho Mtakatifu na Miujiza

Mungu alitenda miujiza mingi katika siku za Biblia kupitia watumishi wake kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Kusudi kuu la miujiza lilikuwa uthibitisho wa Neno la Mungu (Mt. 9:4-5; 12:28-29; Mk. 2:10-11; 16:17-20; Lk. 5:24; Yn. 21:24-25; Mdo. 2:32-33; 2 Kor 12:12). Kuhusiana na wokovu mkuu ambao Mungu amewapa wanadamu, mwandishi wa Waebrania alisema,"***kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia; Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenyewe***" (Ebr. 2:3-4). Mara ufunuo wa Mungu katika Kristo ulipojulikana kikamilifu, miujiza ilikuwa imetimiza kusudi lake kuu. Wakati wa karne ya kwanza kupungua kwa matukio ya miujiza kulionekana, na kufikia karne ya pili miujiza haikufanyika tena.

Madai ya kisasa ya miujiza yanayofanywa na watu wa dini, wakristo na wasio wakristo, ni dhaifu ukilinganisha na miujiza ya kweli ya historia ya Agano Jipya. Wakati fulani madai ya kisasa ya miujiza ni uponyaji wa kisaikolojia tu. Wakati mwingine linakuwa tukio lisilo la kawaida tu badala ya kuwa tukio linalozidi uwezo wa kufikiri kwa mwanadamu. Madai mengine ya kisasa ya miujiza yanaweza kuelezewa kwa urahisi kama matukio ya asili, kwa mfano, dai la kisasa la kunena kwa lugha halihusiani na karama za Agano Jipya. Kunena kwa lugha katika Agano Jipya kulikuwa ni kunena kwa lugha ya kigeni [ya watu] ambayo mtu hakuwahi kujifunza kamwe (Mdo. 2:6,8).

Kunena kwa lugha kwa kisasa si lolote zaidi ya matamshi ya watoto wachanga ambayo wataalam wa lugha wanasema si lugha halisi na pia wanasaikolojia wanasema kunena huko kunatekelezwa na watu wenye sifa fulani za kibinafsi, mara nyingi ni zenye mvuto kwa watu. Madai mengi ya kisasa ya kufanya miujiza ni matokeo ya udanganyifu na hila za wasanii wasio waaminifu. Wanawinda ujinga

wawatu au matumaini ya watu walemavu au wagonjwa sana. Uchunguzi mwingi wa wanasayansi wasiopendelea upande wowote wameshindwa kuwagundua wafanya miujiza wa kweli katika ulimwengu wa leo. Wakati huo huo simu nyingi zimewekwa wazi. Hakuna mtu leo aliye na uwezo wa kufanya miujiza, kuponya wagonjwa, kunena kwa lugha, au kufufua wafu.

Mungu hakupanga miujiza iendelee katika vipindi vyote. Kazi ya miujiza ilikuwa kulithibitisha Neno na kusaidia kuanzisha mpango wake wa ukombozi. Mara tu hilo lilipofanywa, Mungu hakutaka watu wategemee mkongojo ili kuamini. Alitaka watu, "***waenende kwa imani, si kwa kuona***" (2 Kor. 5:7). Mara baada ya kanisa kupata ujumbe uliothibitishwa na mara baada ya kumbukubu ya kudumu nay a kutegemewa kuandikwa, yaani maandiko ya Agano Jipya, Mungu aliacha miujiza ipungue na hatimaye ikome kabisa. mchakato huu ulitoa nafasi kwa kanisa kuwa kitu kizima na kukua, likitenda kama mtu mzima anayetembea katika imani, badala ya mtoto anayehitaji muujizakwa ajili ya uthibitisho. Paulo alirejelea hili kama ujio wa "ukamilifu" (1 Kor. 13:8-13, ling: Efe. 4:11-16). Kuomba miujizaleo ni kurudi katika hali ya utoto (Mt. 12:38-39; 1 Kor. 13:11). Hata karama za miujiza zilipokuwepo katika kanisa la Agano Jipya, Paulo alibainisha umuhimu wake mdogo na kusisitiza umuhimu mkubwa wa upendo katika maisha yetu (1 Kor. 12:29-13:13). Kilichopaswa kudumu katika kipindi chote cha Ukristo kilikuwa imani, tumaini, na upendo, kama Paulo alivyoeleza katika kifungu hiki, "***Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo***" (1 Kor. 13:13; ling Mt. 22:36-40).

# Maandiko Matakatifu

Nyaraka zinazounda maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya, Biblia, zinachukuliwa kuwa na mamlaka kwa Wakristo. Hizo ndiyo mahakama kuu ya mwisho ambayo mtu anaweza kuiendea ili aweze kujibu swali lolote la kidini. Biblia inatufunulia mapenzi ya Mungu na kumbukumbu zote jinsi Mungu alivyotenda katika historia kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu (Zab. 119:105). Waandishi wa maandiko walisaidiwa na Roho Mtakatifu katika uandishi wao, kwa hiyo Biblia si kitabu cha kawaida. Imevuviwa, yaani, iko haì pamoja na Roho Mtakatifu na inaweza kumwongoza mtu kuelekea kwenye uzima wa milele (Ebr. 4:12). Chanzo au asili ya maandiko ni Mungu mwenyewe. Maandishi haya si maoni tu au tafsiri za waandishi (2 Pet. 1:20-21). Kama Paulo alivyosema, "***Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema***" (2 Tim 3:16-17). Vitabu vingine isipokuwa Biblia vinaweza kusomwa, kwa faida yetu au hasara yetu. Hata hivyo, kusoma Biblia, kuiamini, na kuitii kunamaanisha wokovu (Yak. 1:21; 2 Tim. 3:15; 1 Pet. 1:22-25; Yn. 20:30-31).

Biblia ni mkusanyiko wa vitabu sitini na sita tofauti vyenye urefu unaotofautiana kutoka kwa waandishi wapatao arobaini vilivyoandikwa kwa zaidi ya miaka 1500. Biblia imegawanyika katika sehemu kuu mbili, Agano la Kale na Agano Jipya. Maandiko ya Agano la Kale yaliandikwa wakati wa kipindi cha Musa. Yamebeba maelekezo yanayowataka Waisraeli wajue jinsi ya kuishi na kuabudu. Pia yana historia, mashairi, nyimbo za ibada, maneno ya hekima, na matangazo ya kinabii. Wakristo wanaamini katika maandiko ya Agano la Kale kama ufunuo uliovuviwa wa mapenzi ya Mungu (2 Tim. 3:16; 2 Pet. 1:21; Yn.

10:35), lakini hatufuati amri zote za kidini zinazopatikana humo. Amri hizi zilitolewa kwa waisraeli kwa ajili wakati wa kipindi cha Musa(Kum. 5:12; Eze. 20:10-12). Yesu Kristo ameleta historia mpya (Mt. 5:17; Kol. 2:14; Efe. 2:15; Rum. 6:14; 7:4; 10:4). Agano la Kale lilikuwa ni maandalizi kwa ajili ya Agano Jipya, na Wakristo wanaishi chini ya Agano Jipya (Gal. 3:23-26; Ebr. 7:12; 8:1-13; 10:1-10; Kol. 2:14). Kwa mfano, wakristo hawatoi dhabihu za wanyama, kwa sababu Kristo ni dhabihu yetu iliyotolewa mara moja kwa ajili wote.

Ijapokuwa wakristo hawaishi chini ya sheria ya Musa, kuna sababu nyingi za kusoma maandishi ya Agano la Kale. Kanisa la awali lilihubiri kutoka katika Agano la Kale, lilinukuu, na hata kujifunza kutoka katika Agano la Kale (Mdo. 2:14-36; 8:31-35; 17:2-3,11; 18:28; 28:23). Paulo alithibitisha kwamba liliwafaa na liliwasaidia wakristo (1 Kor. 10:11; Rum. 15:4). Kanuni nyingi asili yake ni Agano la Kale. Sifa nzurina sifa mbaya zinaonyeshwa katika maisha ya wahusika wa Agano la Kale. Ni kumbukumbu muhimu ya kihistoria. Lnaelezea mambo mengi yaliyo katika Agano Jipya, nalinamshuhudia Yesu Kristo. Jifunze vitabu vya Agano la Kale iliujue ukweli mkuu kuhusu tabia ya Mungu na jinsi ya kuishi maisha mazuri na ya kimaadili. Lakini kuwa mwangalifu usifuate majukumu ya kidini wa Agano la Kale ambayo yalikusudiwa kwa Waisraeli peke yao (Gal. 5:4).

Maandishi ya Agano Jipya ni muhimu, kwa sababu yanaeleza habari za Yesu na kanisa la awali. Maana ya ufunuo wa Mungu katika Yesu Kristo imefafanuliwa katika maandiko ya Agano Jipya. Agano Jipya lina hati ambazo zinasimama katika nafasi ya kipekee ya kihistoria, kwa sababu ziliandikwa na watu ambao walikuwa mashahidi wa maisha, miujiza, kifo na ufufuo wa Yesu Kristo. Vitabu vingi vya Agano Jipya viliandikwa na mitume wa Yesu waliochaguliwa maalum (Rum. 1:1; Gal. 1:1; 1 Pet. 1:1; 2 Pet. 1:1). Katika kusoma Biblia inashauriwa mtu

aanze na Injili kisha asome Agano Jipya lote kabla ya kusoma Agano la Kale.

# Muhtasari wa Vitabu vya Biblia

## *Maandiko ya Agano la Kale*

**Mwanzo**: Historia ya mwanzo wa ulimwengu, jamii ya wanadamu, na shughuli za awali za Mungu na wanadamu kupitia Kipindi cha Mababa. Vitabu vitano vya kwanza vya Agano la Kale vinaitwa Torati.

**Kutoka**: Ukombozi wa Israeli kutoka utumwani Misri.

**Mambo Ya Walawi**: Sheria za sikukuu, za kijamii na za maadili kwa Israeli.

**Hesabu:** Kumbukumbu ya kutangatanga kwa Israeli jangwani.

**Kumbukumbu La Torati**: Agano la sheria kati ya Mungu na Israeli.

**Yoshua**: Kutekwa na kugawanywa kwa nchi ya ahadi na kwa makabila ya Israeli.

**Waamuzi**: Historia ya Israeli kabla ya ufalme.

**Ruthu**: Hadithi ya nyanya wa mfalme Daudi.

**1 Samweli**: Maisha ya Samweli, Sauli na Daudi.

**2 Samweli**: Habari zaidi za maisha ya Daudi, mfalme wa pili wa Israeli.

**1 Wafalme**: Maisha ya Sulemani na wafalme wengine na sehemu ya maisha ya nabii Eliya.

**2 Wafalme**: Eliya na Elisha na historia za falme za Israeli na Yuda hadi utumwani Babeli.

**1 Mambo Ya Nyakati**: Nasaba na simulizi za utawala wa Daudi.

**2 Mambo Ya Nyakati**: Simulizi za utawala wa Sulemani na wafalme wengine hadi maangamizi ya Yerusalemu yaliyotekelezwa na Babeli.

**Ezra**: Kurudi kwa waisraeli kutoka Babeli, kujengwa upya kwa hekalu, na kazi ya Ezra.

**Nehemia**: Ujenzi mpya wa kuta za Yerusalemu chini ya uongozi wa Nehemia.

**Esta**: Wokovu wa Wayahudu na Esta kipindi cha Uajemi.

**Ayubu**: Majadiliano juu ya haki ya Mungu mtu mwenye haki anaporuhusiwa kuteseka.

**Zaburi**: Mkusanyiko wa nyimbo na maombi ya Waisraeli.

**Mithali:** Mkusanyiko wa misemo ya hekima, mingi iliandikwa na Sulemani.

**Mhubiri**: Mjadala juu ya maana na madhumuni ya maisha.

**Wimbo Ulio Bora**: Shairi linalohusu upendo.

**Isaya**: Mausia ya kinabii kuhusu ufalme mkuu wa Mungu na tumaini la Masihi. Kitabu hiki nahivyo vinavyofuata ni uandishi wa kinabii.

**Yeremia**: Matangazo ya kinabii, hasa juu ya kuanguka kwa Yuda mikononi mwa Babeli.

**Maombolezo**: Maombolezo juu ya kuanguka kwa Yerusalemu mikononi mwa Babeli.

**Ezekieli**: Mtazamowa kinabii kutoka Babeli juu ya kuanguka kwa Yuda mikononi mwa Babeli na marejesho ya mwisho.

**Danieli**: Baadhi ya matukio wakati wa utumwa wa Babeli na uthibitisho wa udhibiti wa Mungu na wa historia.

**Hosea**: Ukosefu wa uaminifu wa Israeli na upendo wa Mungu, umeelezewa kwa sehemu katika ndoa ya Hosea na Gomeri.

**Yoeli**: Wito wa toba kufuatia pigo la nzige.

**Amosi**: Wito wakwa ajili ya haki ya kijamii katika Israeli.

**Obadia**: Edomu ilihukumiwa kwa kufurahia maafa ya Israeli.

**Yona**: Nabii mwenye kusitasita anahubiri katika mji la Ninawi.

**Mika**: Shutuma juu ya ukosefu wa haki, matambiko ya bure na maelezo kuhusu dini ya kweli.

**Nahumu**: Tangazo la enzi kuu ya Mungu kama inavyoonekana katika hukumu yake juu ya Ninawi.

**Habakuki**: Imani katika haki ya Mungu iliyopingwa na ukandamizaji kwa maskini na ustawi wa watu waovu.

**Sefania**: Hukumu ya Mungu juu ya dhambi za Yuda na mataifa mengine.

**Hagai**: Kuwatia moyo wayahudi ili waweze wajenge upya hekalu.

**Zekaria**: Kujengwa upya kwa hekalu na tumaini la Masihi.

**Malaki**: Himizo kwaajili ya Israeli wenye dhambi kutubu.

## Maandiko ya Agano Jipya

**Mathayo**: Injili ya kwanza kati ya Injili nne inayoeleza kuhusu maisha na mafundisho ya Yesu Kristo.

**Marko**: Injili fupi kati ya injili nne ambayo inatilia mkazo matendo zaidi kuliko mafundisho ya Yesu.

**Luka**: Injili inayoonyesha upendo wa Yesu wa ulimwengu mzima kwa kila aina ya watu.

**Yohana**: Injili ya mwisho kuandikwa na imeundwa kuwaleta wasomaji wake kwenye imani ya Yesu.

**Matendo ya Mitume**: Historia ya kanisa la awali ambayo inaelezea zaidi kazi ya mitume, Petro na Paulo.

**Warumi**: Moja ya nyaraka kumi na tatu za Mtume Paulo zinazoeleza mpango wa Mungu wa wokovu kwa njia ya Yesu Kristo.

**1 Wakorintho**: Jaribio la kurekebisha matatizo katika kanisa la Korintho.

**2 Wakorintho**: Kujitetea kwa Paulo juu yake mwenyewe na utume wake.

**Wagalatia**: Utetezi wa kuhesabiwa haki kwa imani dhidi ya majaribio ya kuingiza ibada za kiyahudi kwenye kanisa.

**Waefeso**: Maelezo ya kusudi la Mungu la milele katika Kristo na Kanisa.

**Wafilipi**: Furaha ya Injili na shukrani za Paulo.

**Wakolosai**: Uzushi wa mapema uliokanushwa na ukuu na utoshelevu wa Kristo.

**1 Wathesalonike**: Ujio wa pili wa Kristo, maisha ya kanisa na huduma ya Paulo.

**2 Wathesalonike**: Himizo la kuendelea kufanya kazi mpaka Kristo atakaporudi.

**1 Timotheo**: Barua ya kutia moyo kwa mhubiri kijana aliyekabiliwa na matatizo na pamoja na walimu wa uongo.

**2 Timotheo**: Barua nyingine ya kutia moyo kwa Timotheo muda mfupi kabla ya kifo cha Paulo.

**Tito**: Mwongozo kwaajili ya mhubiri kijana mwingine.

**Filemoni**: Jaribio la kuwapatanisha mtumwa mtoro aliyeongoka karibuna Bwana wake Mkristo.

**Waebrania**: Ubora wa Kristo kama kuhani mkuu na ubora wa Injili dhidi ya mfumo wa Agano la Kale.

**Yakobo**: Mafundisho ya vitendo kwa maisha ya Kikristo ya kila siku.

**1 Petro**: Maisha matakatifu katika uso wa mateso yanayoongezeka.

**2 Petro**: Tatizo la walimu wa uongo katika kanisa.

**1 Yohana:** Hakikisho kwa kanisa lililokabiliwa na mafundisho ya uwongo ya unostiki.

**2 Yohana**: Umuhimu wa kuwapenda waaminifu huku tukiwapinga waalimu wa uongo.

**3 Yohana**: Barua ya binafsi ya shukrani.

**Yuda**: Onyo dhidi ya walimu wa uongo.

**Ufunuo**: Hukumu ya lugha ya mfano kwa mtawala wa kirumi kwa kulitesa kanisa la kwanza na unabii juu ya anguko la Rumi na mwisho wa ulimwengu.

## Hitimisho

Ukristo ni nini? Baada ya majadiliano mengi juu ya mada mbalimbali, inatumainiwa kwamba jibu liko wazi. Ukristo ni imani kwamba Yesu wa Nazareti ni mwana wa Mungu, Kristo na Bwana. Ni kuamini kwamba ufunuo wa juu kabisa wa upendo na mapenzi ya Mungu hupatikana ndani yake. Kuwa Mkristo ina maana kwamba "unamjua Kristo" na unakuwa "kama Yeye" mpaka "Kristo aumbike ndani yako" na "aishi" ndani yako (Flp. 3:10; Gal. 2:20; 4:19; ling, Efe. 4:13).Mkristo ni yule ambaye "anaishi kwa imani katika Mwana wa Mungu" (Gal. 2:20). Kumjua Kristo ni muhimu sana kiasi kwamba ukilinganisha na jambo linguine lolote duniani linaonekana kama takataka (Flp. 1:21; 3:7-9), kwa sababu Yesu Kristo ndiye tumaini pekee la wokovu kwa wanadamu (Mdo. 4:12; Yn. 14:6). Umuhimu wa Yesu Kristo umeelezwa vyema na mwandishi wa waraka kwa Waebrania:

"***Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu***" (Ebr. 1:1-3).

MtumePaulo pia aliandika muhtasari mzuri sana kumwonyesha Yesu ni nani: ***“naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au***

***mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye. Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote. Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae; na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni"*** (Kol. 1:15-20).

Neno dogo la Kiyunani "dia" kwa kawaida hutafsiriwa na neno "kupitia". Mara nyingi linatumika kwa wakala, yaani, mtu(kitu) anayesimama kati ya kufikiwa na kutofikiwa kwa kitu au lengo. Angalia katika vifungu vifuatavyo jinsi neema, ukweli, wokovu, uzima, msamaha, amana, kuhesabiwa haki, haki, ushindi dhidi ya kifo, na upatanisho vinavyouja "kupitia" Yesu Kristo (Yn. 1:17; 3:17; 10:9; 14:6; Mdo. 10:43; 13:38; 15:11; Rum. 1:5; 5:1,2,9,17,18,19,21; 8:37; 1 Kor. 15:57; 2 Kor. 3:4; 5:18; Efe. 1:5; 2:18; Flp. 1:11; Kol. 1:20; 1 The. 5:9; Ebr. 7:25; 1 Yoh. 4:9).

Umuhimu wa Yesu unaonekana katika majina mengi, vyeo, na maneno mengi ya ufafanuzi anayopewa katika Biblia, ambayo ni pamoja na Kristo (Mt. 16:16), Mungu (Yn.1:1; 20:28), Mwana wa Mungu (Yn. 3:16; 20:31; Rum. 1:3), Imanueli (Mt. 1:23), Mwana-kondoo wa Mungu (Yn. 1:29), Nuru ya ulimwengu (Yn. 9:5), Mwokozi (Lk. 2:11; Yn. 4:42), Neno (Yn. 1:1,14), Alfa na Omega (Ufu. 21:6), Mchungaji Mwema (Yn. 10:11), Mfalme wa Wayahudi (Mt. 27:37), Bwana (Mdo. 2:36), mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana (Ufu. 19:16), Bwana wa utukufu (1 Kor. 2:8), Mtakatifu wa Mungu (Mk. 12:4), Jiwe la pembeni(Efe. 2:20),Msingi (1 Kor. 3:11), Mchungaji Mkuu (1 Pet. 5:4), na Mwana Mpendwa (Lk. 3:22; 9:35).

Ni kwa sababu hizi tunamsihi msomaji kumwamini Yesu Kristo na kutoa kuwa kwa mapenzi yake. Kuna kila kitu cha kupata, wala hakuna

cha kupoteza. Katika tukio moja watu kadhaa waliacha kumfuata Yesu. Yesu aliwageukia wanafunzi waliosalia na kuwauliza, "***Je, Ninyi nanyi mwataka kuondoka? Basi Simoni Petro akamjibu, Bwana!Twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele. Nasi tumesadiki, tena tumejua, ya kuwa wewe ndiwe Mtakatifu wa Mungu***" (Yn. 6:66-69)**.** Kwa nini kitabu hiki kiliandikwa? Kwa kutumia maneno ya mtume Yohana, kiliandikwa "***ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake***" (Yn. 20:30-31).